**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI (NEEC)**

# TAARIFA YA MAONESHO YA SITA (6) YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI KIUCHUMI YALIYOFANYIKA UWANJA WA MWANGA - KIGOMA

**TAREHE 21-28 MEI 2023**

Kauli Mbiu:
‘‘Uwezeshaji Kiuchumi Kupitia Mabadiliko ya Kidigitali’’

Imeandaliwa Na:

**Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC),**
**Viwanja Vya Nzuguni, Nane-Nane, Block Na. 2, Kitalu A, Barabara ya Kondoa**
**S.L.P 792,**
**DODOMA**

**MEI, 2023**

## YALIYOMO


YALIYOMO ........................................................................................................i
ORODHA YA VIFUPISHO........................................................................................iii
ORODHA YA MICHORO NA MAJEDWALI ...............................................................iv
DIBAJI..................................................................................................................v
MUHTASARI MAHSUSI ............................................................................................ vi

**SURA YA KWANZA .............................................................................................1**
**1. UTANGULIZI..........................................................................................................1**
1.1 WALENGWA WA MAONESHO YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI .. 2
1.2 CHIMBUKO NA HISTORIA YA MAONESHO YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI ..........................................................................................................2
1.3 MADHUMUNI YA MAONESHO.............................................................................4
1.3.1 DHUMUNI KUU ......................................................................................................4
1.3.2 MADHUMUNI MAHSUSI .......................................................................................4

**SURA YA PILI.............................................................................................................5**
**2. UFUNGUZI NA UFUNGAJI WA KILELE CHA MAONESHO YA WIKI YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI .........................................................................5**
2.1 UFUNGUZI WA MAONESHO .................................................................................. 5
2.1.1 VIONGOZI NA WAGENI KUTEMBELEA MABANDA YA MAONESHO ................. 5
2.1.2 SANAA NA BURUDANI........................................................................................... 5
2.1.3 UTAMBULISHO NA MADHUMUNI YA MAONESHO...........................................5
2.1.4 HOTUBA YA UFUNGUZI WA MAONESHO........................................................6
2.2 UFUNGAJI NA HOTUBA YA MGENI RASMI KUHITIMISHA KILELE CHA MAONESHO....................................................................................................................7
2.2.1 UTAMBULISHO NA MADHUMUNI YA MAONESHO ...................................7
2.2.2 SALAAMU ZA MWENYEKITI WA BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI ..... 9
2.2 3 SALAAMU ZA MKOA WA KIGOMA ........................................................................10
2.2.4 SALAAMU ZA MKUU WA MKOA WA TABORA...................................................10
2.2.5 HOTUBA YA MGENI RASMI KUFUNGA KILELE CHA MAONESHO ..................10
2.2.5.1 Mikopo Wakati wa Maonesho.............................................................................. 13
2.2.5.2 Utoaji wa Tuzo za Washindi ................................................................................ 13
2.2.6 NENO LA SHUKRANI KUTOKA WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA ........................................................................................................... 14

**SURA YA TATU..........................................................................................................14**
**3. MATOKEO YA TATHMINI YA MAONESHO YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI............................................................................................................ 15**
3.1 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA TAARIFA ZA MAHUDHURIO............................15
3.1.1 MCHANGANUO WA MAHUDHURIO YA WANANCHI NA WASHIRIKI WA MAONESHO.................................................................................................. 15
3.1.1.1 Idadi ya Wajasiriamali na Taasisi za Utoaji Huduma za Biashara na Fedha ..... 16
3.1.1.2 Idadi ya Waratibu wa Madawati ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ................ 16
3.1.1.3 Idadi ya Washiriki *Exhibotors* Katika Mabanda................................................ 16
3.1.1.4 Idadi ya Wananchi Waliohudumiwa Katika Mabanda ........................................ 17
3.2 MATOKEO YA TATHMINI YA MAKUNDI YA WASHIRIKI WA MAONESHO.......... 17

3.2.1 WAJASIRIAMALI ........................................................................................ 17
3.2.1.1 Taarifa za Ushiriki kwa Wajasiriamali Katika Maonesho .................................... 17
3.2.1.2 Viwango vya Elimu vya Wajasiriamali ................................................................. 18
3.2.1.3 Ujengaji Uwezo wa Mafunzo ya Urasimishaji kwa Wajasiriamali ....................... 20
3.2.1.4 Aina za Biashara za Wajasiriamali na Ushiriki katika Mikoa .............................. 23
3.2.1.5 Ushiriki wa Wajasiriamali, Usajili na Urasimishaji wa Biashara.......................... 24
3.2.1.6 Vyanzo vya Mitaji ya Wajasiriamali .................................................................... 27
3.2.1.7 Mikopo na Marejesho ya Wajasiriamali .............................................................. 28
3.2.1.8 Ajira za Biashara za Wajasiriamali...................................................................... 29
3.2.2 WATOA HUDUMA ZA UENDELEZAJI WA BIASHARA NA FEDHA .................... 30

**SURA YA NNE ................................................................................................ 33**
**4. MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA UTATUZI WA CHANGAMOTO ......................... 33**
4.1 MAFANIKIO YA MAONESHO ............................................................................. 33
4.2 CHANGAMOTO ZA JUMLA NA UTATUZI WA HIZO CHANGAMOTO .................. 34

**SURA YA TANO ................................................................................................ 37**
**5. HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........................................................................ 37**
5.1 HITIMISHO ......................................................................................................... 37
5.2 MAPENDEKEZO ................................................................................................. 38
5.2.1 WAJASIRIAMALI ............................................................................................. 38
5.2.2 MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI ..................................................... 38
5.2.3 WARATIBU WA MADAWATI YA UWEZESHAJI .................................................. 38

**6. VIAMBATISHO**
KIAMBATISHO Na. 1: FOMU YA TATHMINI –MJASIRIAMALI/MSHIRIKI WA MAFUNZO
KIAMBATISHO Na. 2: FOMU YA TATHMINI – MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI
KIAMBATISHO Na. 3: FOMU YA TATHMINI – WATOAJI HUDUMA ZA BIASHARA (BDS) NA TAASISI
KIAMBATISHO Na. 4: FOMU YA TATHMINI – WARATIBU WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AGITF | Mfuko wa Pembejeo za Kilimo |
| AMCOS | Chama cha Ushirika cha Msingi cha Mazao na Masoko |
| BBT | Programu ya Kilimo Biashara kwa Vijana |
| BDS | Huduma za Maendeleo ya Biashara |
| BoT | Benki Kuu ya Tanzania |
| BRELA | Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni |
| CRDB | Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini |
| CSOs | Asasi za Kiraia |
| DECOs | Waratibu wa Halmashauri wa Madawati ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi |
| e-GA | Mamlaka ya Serikali Mtandao |
| EWURA | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji |
| FCC | Tume ya Ushindani |
| FYDP | Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 2025/2026 |
| GS1 (TZ) | *Global System of Standards.* |
| IFM | Chuo cha Usimamizi wa Fedha |
| MoCU | Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi |
| NEDF | Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Ujasiriamali |
| NEEC | Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi |
| NGOs | Mashirika Yasiyo ya Kiserikali |
| NSSF | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii |
| OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| OSHA | Wakala wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi |
| RECOs | Waratibu wa Mikoa wa Madawati ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi |
| SACCOS | Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo |
| SANVN | SIDO, Azania Bank, NSSF, VETA and NEEC |
| SIDO | Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo |
| TAKUKURU | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na rushwa |
| TASAF | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania |
| TADB | Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania |
| TACT | Mfuko wa Kuchochea Kilimo Tanzania |
| TBS | Shirika la Viwango Tanzania |
| TDV | Mpango wa Dira ya Taifa 2025 |
| TIA | Chuo cha Uhasibu Tanzania |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| TTCL | Shirika la Mawasiliano Tanzania |
| UCSAF | Mfuko wa Mawasiliano kwa Umma |
| UTT AMIS | Dhamana ya Uwekezaji na Usimamizi Rasilimali Tanzania |
| YDF | Mfuko wa Maendeleo ya Vijana |
| VETA | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi |
| WMA | Wakala wa Vipimo |

# ORODHA YA MICHORO NA MAJEDWALI

**Orodha ya Majedwali**

Jedwali Na. 1: Mwenendo na Idadi ya Wananchi Waliohudumiwa na Kupata Huduma Katika Mabanda ya Washiriki ........ 3
Jedwali Na. 2: Washindi wa Tuzo kwa Makundi ........ 13
Jedwali Na 3: Machanganuo wa Mahudhurio ya Wananchi na Washiriki wa Maonesho........ 15
Jedwali Na. 4: Idadi ya Wajasiriamali Walionufaika na Mafunzo ya Urasimishaji........ 21
Jedwali Na. 5: Matokeo ya Tathmini ya Mafunzo kwa Wajasiriamali........ 22
Jedwali Na. 6: Idadi ya Wajasiriamali wa Maonesho Kimkoa ........ 23
Jedwali Na. 7: Aina za Biashara Wajasiriamali........ 23
Jedwali Na 8: Mtaji wa Biashara wa Hapo Awali na Hadi Mei, 2023 ........ 28

## Orodha ya Michoro

Mchoro Na. 1: Idadi ya Washiriki Waoneshaji wa Maonesho katika Mabanda ........ 16
Mchoro Na. 2: Idadi ya Wananchi Waliohudumiwa Katika Mabanda ........ 17
Mchoro Na. 3: Vyanzo vya Taarifa za Maonesho ........ 18
Mchoro Na. 4: Viwango vya Elimu vya Wajasiriamali ........ 19
Mchoro Na.5: Viwango vya Elimu vya Wajasiriamali........ 20
Mchoro Na. 6: Idadi ya Wajasiriamali wa Maonesho Kimkoa ........ 23
Mchoro Na. 7: Muda wa Biashara za Wajasiriamali........ 24
Mchoro Na. 8: Ushiriki wa Wajasiriamali katika Mikoa ........ 25
Mchoro Na. 9: Biashara Rasmi na Zisizo Rasmi ........ 26
Mchoro Na. 10: Vyanzo vya Mitaji vya Wajasiriamali wa Maonesho........ 27
Mchoro Na. 11: Muda wa Marejesho ya Mikopo ........ 29
Mchoro Na. 12: Hali ya Ajira katika Biashara za Wajasiriamali ........ 30
Michoro Na. 13: Aina ya Huduma za Taasisi katika Maonesho........ 31
Mchoro Na. 14: Maombi ya Mikopo na Dhamana........ 32

## DIBAJI

Ninayo furaha ya kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita (6) chini ya uongozi mahiri wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuendeleza jitihada za uwezeshaji wananchi kiuchumi ikiwa ni pamoja na maonesho ya mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji yalianza kufanyika mwaka 2017 na yamekuwa na mwendelezo wa kufanyika kila mwaka ambapo katika mwaka 2023 yamefanyika mkoani Kigoma kwa kanda ya magharibi.

Maonesho ya sita (6) ya mifuko na programu za uwezeshaji yalishirikisha wadau kutoka sekta mbalimbali za kiuchumi. Maonesho haya ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 ambayo inalenga kuendeleza jitihada za Serikali katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 tuliyojiwekea ya kuboresha hali ya maisha ya Watanzania pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya ukuaji wa maendeleo ya sekta binafsi.

Aidha, nichukue fursa hii kuushukuru mkoa wa Kigoma pamoja na viongozi wake kwa ushirikiano wa kuratibu maonesho ya sita ya uwezeshaji wananchi ambayo yaliwezesha wananchi walio wengi kufahamu jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuainisha fursa za mitaji mbalimbali kutoka katika mabenki, mifuko ya uwezeshaji na programu za uwezeshaji. Maonesho yalikuwa na manufaa makubwa kwa kuhamasisha wafanyabiashara na wajasiriamali kurasimisha biashara ikiwa ni njia ya kuongeza usajili wa biashara na hatimaye kuongeza wigo mpana wa walipa kodi kupitia biashara zilizosajiliwa na zinazotambulika.

Niwashukuru pia wachangiaji wa michango kutoka kwa wadau wa taasisi tekelezi za uwezeshaji ambao kwa namna moja ama nyingine michango na mawazo yao yaliwezesha maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji kuratibiwa na kufanyika kwa wakati muafaka. Hivyo, natoa rai tuendelee kushirikiana ili kufanisha juhudi za Serikali kufanikisha mipango na mikakati ya utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) litaendelea kutoa ushirikiano na kuwashirikisha wadau wa sekta ya umma na binafsi ili kufanikisha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Wadau wengine wa uwezeshaji ni pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali, asasi za kiraia, vyuo vya elimu, watafiti, watoa huduma za biashara, vikundi vya kijamii vya fedha, vyama vya ushirika n.k. Mwisho, Baraza litaendelea kutekeleza maelekezo ya viongozi wa nchi kupitia kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Kazi Iendelee, ili kuwezesha kila mdau wa uwezeshaji kutimiza wajibu wake ipasavyo ili kufanikisha utekelezaji madhubuti wa masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ambayo utekelezaji wake ni mtambuka wenye kuhisisha wadau wa sekta mbalimbali za kiuchumi.

CPA, Bibi. Beng’i Issa
**Katibu Mtendaji,**
**NEEC**

## MUHTASARI MAHSUSI

Serikali ya awamu ya sita imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuwezesha wananchi kupata mitaji kupitia fursa za uwekezaji katika mabenki, mifuko na progamu za uwezeshaji. Serikali pia kupitia maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji imeendelea kuhamasisha wananchi kujenga utamaduni wa kuweka akiba kwa wananchi na ununuzi wa hisa kama sehemu za kukuza mitaji. Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi (NEEC) ambayo yanalenga kufanikisha mikakati ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025). Lengo la uwezeshaji pamoja na mambo mengine ni kuhakikisha sehemu kubwa ya uchumi wa Tanzania inamilikiwa na watanzania wenyewe na kutoa fursa ya ukuaji wa maendeleo ya sekta binafsi. Maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji yanalenga pia makundi yenye uwezo mdogo hususani wajasiriamali na wafanyabiashara.

Madhumuni  ya maonesho pamoja na mambo mengine ni kukuza uelewa wa wananchi kuhusu uwepo wa huduma za mifuko na programu za uwezeshaji na hivyo kuwahamasisha wananchi ili waweze kunufaika na fursa zilizopo katika mifuko hiyo. Pia maonesho yalilenga kuhamasisha wananchi kujenga utamaduni wa kuweka akiba na kuwekeza katika miradi yenye kuleta matokeo ya haraka. Sanjari na hayo, maonesho yalilenga katika kuwaunganisha wajasiriamali na masoko ya bidhaa pamoja na kuhamasisha uongezaji ubora wa bidhaa ili ziweze kushindana katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Maonesho vilevile yaliwezesha kuwakutanisha wajasiriamali na watoa huduma za biashara na fedha na hatimaye kujenga mitandao ya kibiashara.

Matokeo ya tathmini yanaonesha maonesho yalihudhuriwa na wananchi na washiriki na wananchi **12,673** huku wanawake wakiwa ni **6,193** na wanaume **6,480.** Sanjari na hayo, mgawanyo wa mahudhurio pia unaonesha wananchi walikuwa **12,167** (wanawake **5,895** na wanaume **6,272**). Wajasiramali walioshiriki ni **185** huku taasisi za Umma na Binafsi zikiwa **43** pamoja na waratibu wa madawati ya uwezeshaji wakiwa **30.**

Matokeo ya tathmini ya mafunzo yanaonyesha kuwa mafunzo haya yamekuwa na tija kwa wajasiriamali kufahamu huduma mbalimbali zitolewazo na taasisi husika za utoaji wa huduma wezeshi za biashara. Mafunzo ya urasimishaji na fursa za mitaji yalitolewa kwa wajasiriamali walioshiriki kwenye maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji. Mafunzo hayo yaliratibiwa na NEEC na kutolewa na taasisi nane (**8**) ambazo ni OSHA, GS1 TZ, SIDO, BRELA, TBS, TRA, NSSF na Azania BANK. Jumla ya wajasiriamali **182** (wanawake **133** na wanaume **52**) kati ya **185** walinufaika na fursa za mafunzo ya kukuza uelewa na kujenga uwezo. Matokeo ya tathmini inaonyesha wajasiriamali **69** (**77.3%)** kati ya **112** wamekiri kuwa wamewahi kushiriki mafunzo ikilinganishwa na wajasiriamali **43 (22.7%)** ambao hawakuwahi kuhudhuria wala kushiriki mafunzo yaliyowaleta taasisi za wezeshi za huduma za biashara pamoja. Maonesho pia yalishuhudia wananchi 203 wakifungua akaunti katika mabenki ya CRDB Bank Plc (**127)** na Azania Bank **(76)** huku maombi **77** yenye thamani ya Tshs **462,364,000** yakiombwa na wajasiriamali walioshiriki maonesho.

Jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi **315,000,000** ilitolewa wakati wa maonesho na taasisi ya fedha ya *SELF Microfinance* ambayo iliidhinisha mkopo wa shilingi

**140,000,000** kwa *Ihacha Credit Microfinance Limited* iliyoko Kigoma huku programu ya SANVN viwanda scheme iliidhinisha mkopo wa shilingi **175,000,000** kwa kiwanda cha *B&L Agridigital* cha alzeti kilichopo Dar es Salaam. Matokeo ya tathmini pia ilibaini maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji mkoani Kigoma yalihudhuriwa na jumla ya wajasiriamali **185** kwa mwaka 2023 iklinganishwa na wajasiriamali **243** warioshiriki maonesho ya mkoa wa Morogoro kwa mwaka 2022. Hivyo, jitihada zinapaswa kufanyika ili kuwezesha ongezeko la ushiriki wa wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa.

Mchango wa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi umekuwa ni mkubwa kwa wananchi hususani wajasiriamali ambao wameendelea kunufaika na fursa za mitaji na kutengeneza ajira kama ilivyoainishwa hapa chini;

- ✓ Takwimu za Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi zinaonesha hadi kufikia Machi, 2023, mifuko na programu za uwezeshaji zimetoa mikopo na dhamana yenye thamani ya shilingi trilioni **6.1** kwa wajasiriamali **8,650,257** wakiwemo wanawake **4,747,321** sawa na asilimia **54.9** na wanaume **3,902,936** sawa na asilimia **45.1.**

- ✓ Mifuko na programu za uwezeshaji imetoa jumla ya ajira **17,603,371** ambapo ajira **9,248,916** ni wanawake sawa na asilimia **52.5** na ajira **8,354,355** ni wanaume sawa na asilimia **47.5.** Mikopo, dhamana na ruzuku zilitolewa katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, viwanda na biashara, utalii, misitu, sanaa, utamaduni na michezo.

Maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji ni muhimu kwa ukuaji wa maendeleo ya sekta binafsi na hatimaye kutengeneza ajira za watanzania pamoja na kufanikisha ukuaji wa pato la taifa. Maonesho pia ni muhimu katika kuwaunganisha wajasiriamali na fursa mbalimbali za masoko, mitaji, elimu, ubunifu, teknolojia, urasimishaji wa biashara n.k. Hivyo, kuna haja ya kuhakikisha ushiriki wa taasisi za utafiti, mafunzo na ubunifu unaongezeka ili kuwezesha kuwaunganisha wananchi na fursa zilizopo katika taasisi wezeshi.

# SURA YA KWANZA

## 1. UTANGULIZI

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan iliendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 kwa kuandaa na kuratibu wiki ya maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi mkoani Kigoma. Maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambayo inalenga zaidi maeneo yenye kuleta matokeo ya haraka hasa yale yanayogusa maisha ya wananchi wenye ujasiriamali katika kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu, ujenzi, biashara, utalii, madini, viwanda, na usafirishaji pamoja na wadau wa kisekta. Maonesho ya saba (7) ya programu na mifuko ya uwezeshaji yaliratibiwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) kwa kushirikiana na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, taasisi tekelezi za mifuko na programu za uwezeshaji pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kigoma.

Maonesho haya yamekuwa yakifanyika kikanda kila mwaka tangu kuasisiwa kwake na yamekuwa ni mwendelezo wa maonesho ya kwanza yaliyozinduliwa mwaka 2017 mkoani Dodoma na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa (Mb). Maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji yamekuwa na manufaa katika kukuza uelewa kwa wananchi na kuwaunganisha na fursa mbalimbali ikiwemo mitaji kupitia mikopo, dhamana na ruzuku; elimu na mafunzo, teknolojia, masoko kutoka taasisi wezeshi. Maonesho ya Saba (7) yalifanyika kanda ya magharibi katika mkoa wa Kigoma katika viwanja vya Mwanga kuanzia tarehe 21 Mei, 2023 hadi 28 Mei, 2023. Maonesho yalifunguliwa na Mkuu wa Wilaya wa Kigoma Mhe. Salum Kalli tarehe 24 Mei, 2023 na kufungwa na Mgeni Rasmi Mkuu wa Mkoa wa Mkoa wa Kigoma Kamishna Mstaafu wa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji Mheshimiwa Thobias Andengenye tarehe 28 Mei, 2023.

> Maonesho yalikuwa na kaulimbiu ***"Uwezeshaji Kiuchumi kupitia Mabadiliko ya Kidigitali".*** Kaulimbiu hii ililenga kuhamasisha mabadiliko ya uhuishaji wa mifumo ya kidigitali ili kuongeza tija na ufanisi wa utoaji wa huduma bora za mifuko na programu za uwezeshaji kwa wananchi.

Maonesho yalihudhuriwa na jumla ya wananchi **12,673** huku wanawake wakiwa ni **6,193** na wanaume **6,480.** Mgawanyo wa mahudhurio pia unaonesha wananchi walikuwa **12,167 (**wanawake **5,895** na wanaume **6272**), wajasiriamali **185** (wanawake **108** na wanaume **77**) na washiriki wa mifuko ya uwezeshaji **291** (wanawake **172** na wanaume **119**) kutoka katika taasisi **73** huku za umma zikiwa ni **45** na kutoka sekta binafsi **27** zilizoshiriki maonesho. Maonesho pia yalihudhuriwa viongozi kutoka katika wizara, mikoa, wilaya, halmashauri, wakuu wa taasisi za Umma na Binafsi na vyama vya siasa. Aidha, maonesho yalihudhuriwa na waratibu wa madawati ya uwezeshaji **30** (wanawake **23** na wanaume **7**) ambao ngazi ya mikoa walikuwa ni wanne (**4**) kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Geita, Kilimanjaro na Kigoma na waratibu wa halmashauri **26**.

Sanjari na hayo, maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji yamekuwa na

mchango mkubwa katika kupanua wigo wa utoaji huduma za kifedha pamoja na huduma nyingine za uwezeshaji ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu kwa umma na mafunzo kwa wajasiriamali. Maonesho ya mkoani Kigoma pamoja na mambo mengine yamekuwa na manufaa mbalimbali ambayo ni:

- Mafunzo ya kujenga uelewa wa urasimishaji na fursa za mitaji yalitolewa kwa wajasiriamali walioshiriki wa maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji. Mafunzo hayo yaliratibiwa na NEEC na kutolewa na taasisi nane (**8**) ambazo ni **OSHA, GS1 TZ, SIDO, BRELA, TBS, TRA, NSSF** na **Azania BANK**. Jumla ya wajasiriamali **182** (wanawake **133** na wanaume **52**) kati ya **185** walinufaika na fursa za mafunzo ya kukuza uelewa na kujenga uwezo.

- Maonesho yalishuhudia jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi **315,000,000** ilitolewa na taasisi ya fedha ya SELF Microfinance ambayo iliidhinisha mkopo wa shilingi **140,000,000** kwa mjasiriamali huku programu ya SANVN nayo ikiidhinisha mkopo wa shilingi **175,000,000** kwa kiwanda cha alzeti.

Sanjari na hayo, maonesho ya wiki ya mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi yamekuwa na mchango chanya katika uendelezaji wa kuipa nafasi kubwa zaidi sekta binafsi kwa kuzingatia masharti ya kuendesha uchumi katika mazingira ya nguvu ya soko. Aidha, mbinu na mikakati inayotumika katika uwezeshaji wananchi kiuchumi inatambua mchango wa sekta isiyo rasmi na kuchukua hatua za kuiboresha na kuishirikisha katika maonesho kama sehemu ya kuchochea urasimishaji, ushindani na ukuaji wa biashara, viwanda na uwekezaji kwa ujumla.

## 1.1 WALENGWA WA MAONESHO YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI

Walengwa wa maonesho ni makampuni ya wananchi ambayo yamesajiliwa Tanzania na walengwa wanamiliki asilimia isiyopungua hamsini ya hisa zote za makampuni hayo, wawekezaji, wawekezaji, wadau wa seka isiyo rasmi, Asasi za Kiraia (CSOs), Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs), wajasiraiamali, watafiti na vyuo vya elimu, watoa huduma za biashara, mabenki, mifuko na programu za uwezeshaji, waratibu wa madawati ya uwezeshaji, wizara, taasisi za Umma. Maonesho pia hujumuisha wakulima, wafugaji, wavuvi, wafanyakazi na wafanyabiashara, na makundi mengine kutoka sekta mbalimbali za kiuchumi. Maonesho ya uwezeshaji ni sehemu ya utekelezaji wa mikakati ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004.

## 1.2 CHIMBUKO NA HISTORIA YA MAONESHO YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI

Chimbuko la mifuko na programu za uwezeshaji linatokana na kutungwa kwa Sera na Sheria Na. 16 ya mwaka 2004 ambayo imelipa Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi (NEEC) jukumu la kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi ikiwemo uratibu na ufuatiliaji wa mifuko na programu za uwezeshaji. Kazi zingine za msingi za Baraza kwa mujibu wa Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Na. 16 ya mwaka 2004 ni

- Kuwapa watanzania fursa za kushiriki katika shughuli za kiuchumi;

- Kukuza na kusaidia shughuli za kiuchumi zinazoanzishwa na kuendeshwa na watanzania;
- Kuhimiza watanzania kuweka akiba na kuwekeza katika shughuli za kiuchumi na
- Kuainisha vyanzo vya fedha kwa ajili ya uwezeshaji wananchi kiuchumi;

Aidha, katika muundo wa uratibu wa mifuko na programu za uwezeshaji, Baraza limekuwa na utaratibu wa kukutana na mifuko ya uwezeshaji mara mbili kila mwaka kwa lengo la kujadili taarifa za utekelezaji za mifuko na programu za uwezeshaji. Vikao hivi vimekuwa na mchango mkubwa ambapo wazo la kuwa na maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji lilizaliwa tarehe 25 Mei, 2015 katika kikao cha wakuu wa Taasisi za Mifuko kilichofanyika ukumbi wa mikutano wa Ofisi za Tume ya Mipango jijini Dar es Salaam. Wazo la maonesho lilitokana na changamoto iliyowasilishwa na wakuu wa taasisi kuwa mifuko na programu za uwezeshaji hazifahamiki kwa wananchi walio wengi hivyo uwepo wa maonesho utaongeza uwazi na uwajibikaji katika kuwanufaisha wananchi. Aidha, utekelezaji wa wazo hili ulipewa nguvu na maelekezo ya Serikali yaliyotolewa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) mwaka 2017 katika maonesho ya kwanza ambapo aliagiza maonesho yafanyike kwa kanda kila mwaka na kuratibiwa na NEEC ili kutoa fursa kwa wananchi kushiriki na kuainisha fursa za uwezeshaji.

Maonesho ya kwanza yalifanyika mwaka 2017 katika Kanda ya Kati iliyohusisha Mikoa wa **Dodoma,** Singida na Tabora; Maonesho ya pili (2) yalifanyika mwaka 2018 katika Kanda ya Nyanda za Juu iliyohusisha Mkoa wa Iringa, **Mbeya,** Njombe, Rukwa, Ruvuma na Songwe; Maonesho ya tatu (3) yalifanyika Mwaka 2019 katika Kanda ya Ziwa na yalihusisha Mkoa wa Geita, Kagera, Mara, Mwanza, **Simiyu** na Shinyanga; Maonesho ya nne (4) yalifanyika mwaka 2021 katika Kanda ya Kaskazini iliyohusisha Mkoa wa **Arusha,** Kilimanjaro, Manyara na Tanga; na Maonesho ya Tano yalifanyika mwaka 2022 katika kanda ya Mashariki iliyohusisha Mkoa wa **Morogoro,** Pwani, Dar es Salaam, Lindi na Mtwara.

**Jedwali Na. 1: Mwenendo na Idadi ya Wananchi Waliohudumiwa na Kupata Huduma Katika Mabanda ya Washiriki**

| Tarehe | Mkoa / (Uwanja) | Kanda | Taasisi Zilizoshiriki | Mahudhurio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | KE | ME | Jumla |
| 18 - 22 Aprili 2017 | Dodoma (Mashujaa) | Kanda ya Kati | **38** | **-** | **-** | **1,945** |
| 19 – 23 Oktoba 2018 | Mbeya (Luanda Nzovye) | Nyanda za Juu Kusini | **46** | **-** | **-** | **1,967** |
| 14 – 20 Oktoba, 2019 | Simiyu (Bariadi) | Kanda ya Ziwa | **44** | **-** | **-** | **2,681** |
| 07 - 13 Februari 2021 | Arusha (Sheikh Amri Abeid) | Kanda ya Kaskazini | **78** | **-** | **-** | **3,090** |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 08 - 14 Mei 2022 | Morogoro (Jamhuri) | Kanda ya Mashariki | **86** | **1,239** | **590** | **1829**[1] |
| 21-27 Mei 2023 | Kigoma (Mwanga) | Kanda ya Magharibi | **73** | **6,193** | **6,480** | **12,673** |
| **Jumla** | | | | **6,372** | **6,644** | **12,916** |

Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji, NEEC 2023**

Kwa sasa mifuko ya uwezeshaji imefikia **73** huku mifuko **63** ikiwa inasimamiwa na Serikali na **10** inamilikiwa na sekta binafsi. Mifuko na programu za uwezeshaji zinatoa huduma za mikopo ya moja kwa moja, dhamana na ruzuku. Mifuko hii inatoa huduma katika sekta mbalimbali za kiuchumi mfano wa hizo sekta ni biashara, kilimo, mifugo na uvuvi, ujenzi, utalii, madini, n.k.

## 1.3 MADHUMUNI YA MAONESHO

### 1.3.1 DHUMUNI KUU

Dhumuni kuu la maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji ni kuelimisha Umma kuhusu jitihada zinazofanywa na wadau wa uwezeshaji wa sekta ya Umma na Binafsi ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha wananchi na wajasiriamali kunufaika na upatikanaji wa fursa za mikopo, dhamana, ruzuku, teknolojia taarifa, masoko, elimu na mafunzo ya ujasiriamali kwa wajasiriamali.

### 1.3.2 MADHUMUNI MAHSUSI

Madhumuni mahsusi ya wiki ya maonesho ya programu na mifuko ya uwezeshaji pamoja na mambo mengine ni

i. Kutatua changamoto zinazozuia wananchi kushiriki kikamilifu katika kukuza uchumi
ii. Kukuza uelewa kwa wananchi walio wengi kufahamu huduma zinazotolewa na mifuko na programu za uwezeshaji wananchi na kuwapa wananchi hamasa ya kujiunga katika vikundi na kufungua kampuni ili kuweza kunufaika.
iii. Kuhamasisha watu kujenga utamaduni wa kuweka akiba na uwekezaji wa miradi;
iv. Kuhimiza uanzishaji na uimarishaji wa vikundi vya Fedha vya Kijamii kwa madhumuni ya kuweka akiba na mtaji ya uwekezaji
v. Kuunganisha wajasiriamali (SMEs) na taasisi wezeshi za huduma za biashara kwa lengo la kuwezesha urasimishaji wa biashara zilizo katika mfumo usio rasmi wa biashara.

[1] Mahudhurio ya Wajasiriamali Walioshiriki Maonesho ya mwaka 2022 Mkoani Morogoro Hayakuonesha Idadi ya Wananchi Waliotembelea Mabanda

# SURA YA PILI

## 2. UFUNGUZI NA UFUNGAJI WA KILELE CHA MAONESHO YA WIKI YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI

### 2.1 UFUNGUZI WA MAONESHO

#### 2.1.1 VIONGOZI NA WAGENI KUTEMBELEA MABANDA YA MAONESHO

Mabanda **93** kati ya **134** (taasisi **43,** waratibu wa madawati ya uwezeshaji **30** na wajasiriamali **185)** yalifanikiwa kutembelewa na viongozi wa Serikali, Chama, Dini na wadau wa sekta binafsi na kupata maelezo ya huduma ama bidhaa zinazopatikana katika mabanda. Matembezi ya kutembelea mabanda yaliongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Kigoma ambaye pia alifungua maonesho ya sita ya mifuko na programu za uwezeshaji katika viwanja vya mwanga.




*Picha hapa chini inamuonesha Mkuu wa wilaya ya Kigoma Hamis Kalli, (wa pili kulia) akiwa na Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la uwezeshaji wananchi kiuchumi (NEEC) Bibi. Beng'i Issa (wa tatu kulia) akipokea zawadi wakati alipotembelea banda la Benki ya maendeleo ya wakulima (TADB) wakati wa ufunguzi wa maonesho ya sita ya mifuko ya Programu ya uwezeshaji wananchi kiuchumi yaliyofanyika katika mkoa wa Kigoma.*

#### 2.1.2 SANAA NA BURUDANI

Maonesho yalishirikisha wasanii ambao walitoa burudani kwa wananchi na viongozi wakati wa maonesho ya uwezeshaji. Wasanii hao ni Kikundi cha AMCOS Bitale Mkongole kilichopo Kigoma vijijini ambacho kilitoa burudani ya ngoma ya asili ya msakatule. AMCOS hii ni mnufaika wa mkopo uliotolewa na Azania Bank kupitia dhamana ya mikopo iliyotolewa na PASS Trust Fund. Kikundi kingine cha ngoma cha Sembe Safi kilitoa burudani za ngoma za asili za mkoa wa Kigoma. Sambamba na hivyo vikundi, mchekeshaji maarufu wa kuigiza sauti za viongozi waandamizi wa nchi Msanii Oscar Nyerere ni miongoni mwa wachekeshaji mahiri waliotoa burudani kwa wananchi na viongozi waliohudhuria wakati wa maonesho.

#### 2.1.3 UTAMBULISHO NA MADHUMUNI YA MAONESHO

Katibu Mtendaji wa NEEC Bibi. Beng'i Issa alianza kwa kuushukuru Mkoa wa Kigoma kwa ushirikiano ulioneshwa wa kuratibu maonesho ambayo ni muhimu kwa wananchi kufahamu jitihada na fursa za uwezeshaji. Katibu Mtendaji katika hotuba yake alizishukuru taasisi zote pamoja na wajasiriamali kwa ushiriki wao licha ya baadhi ya

taasisi na wajasiriamali kutoka mikoa mingine mbali na wale wadau wa Kigoma. Maonesho yalihudhuriwa na jumla ya washiriki waoneshaji **228** ambapo taasisi zilikuwa ni **43** na wajasiriamali **185.** Maonesho vilevile yalihudhuriwa na waratibu wa madawati ya uwezeshaji **30**. Madhumuni ya maonesho yalikuwa ni kukuza uelewa kwa wananchi walio wengi kufahamu huduma zinazotolewa na mifuko na programu za uwezeshaji wananchi na kuwapa wananchi hamasa ya kujiunga katika vikundi na kufungua kampuni ili kuweza kunufaika.

Hotuba ya Katibu Mtendaji pamoja na mambo mengine pia alizungumzia uwepo wa mifuko umewezesha kubaini yafuatayo:

- Uwepo wa mifuko **73** ambayo mifuko **63** inasimamiwa na Sekta ya Umma na 10 ni ya sekta binafsi. Mifuko na programu hizo ni ile inayotoa mikopo ya moja kwa moja, dhamana na ruzuku.

- Zaidi ya Mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni **6.1** imetolewa kwa wajasiriamali na wafanyabiashara kutoka kwenye mifuko na programu sabini na mbili za uwezeshaji wananchi kiuchumi hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2023.

- Mbali na kutoa mikopo hiyo mifuko imeweza kutengeneza ajira milioni **17.6** huku wananwake wakiwa milioni tisa sawa na **53%** ikilinganishwa na wanaume milioni nane sawa na asilimia **47%.**

Aidha, Katibu Mtendaji aliongeza kuwa maonesho hayo katika mkoa wa Kigoma yalilenga kukuza uelewa kwa wananchi walio wengi kufahamu huduma zinazotolewa na mifuko na programu za uwezeshaji wananchi na kuwapa wananchi hamasa ya kujiunga katika vikundi ili kuweza kunufaika.

### 2.1.4 HOTUBA YA UFUNGUZI WA MAONESHO

Maonesho yalifunguliwa tarehe 21 Mei 2023 na Mkuu wa Wilaya ya Kigoma Mhe. Hamis Kalli. Mkuu wa Wilaya katika hotuba yake ya ufunguzi alianza kwa kuwashukuru waandaaji na waratibu wa maonesho ambao ni Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na NEEC kwa uratibu na maandalizi ya maonesho na kwa kuuchagua mkoa wa Kigoma kuwa mwenyeji. Mkuu wa Wilaya pia aliwashukuru viongozi wa mkoa, wilaya na chama kutoka Kigoma. Aidha aliwashukuru wadhamini, wajasiriamali, wananchi na waandashi wa habari kwa kufanya maonesho yaweze kufana. Mkuu wa Wilaya katika ufunguzi wa maonesho hayo alisema maonesho hayo kwa mkoa wa kigoma ni fursa ya wananchi kukuza uchumi wao na kujifunza mambo mazuri yatokanayo na maonesho. Pamoja na hayo, katika kuwapa hamasa wananchi wa mkoa wa Kigoma, Mkuu wa Wilaya alizungumzia mambo yafuatayo:

- Maonesho ni fursa kwa Mkoa wa Kigoma kujifunza namna ya kuwekeza katika kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja, uchumi wa taasisi na Jamii kwa ujumla.
- Manufaa mengine ni kwa wananchi kuainisha fursa zinazotolewa na mifuko ya serikali, huduma msimbilia, huduma za kibenki, kuongeza thamani ya mazao na bidhaa, elimu ya kodi, elimu ya ushirika, elimu kuhusu vyama vya ushirika, elimu

ya vikundi, masuala yahusuyo rushwa, masoko na ithibati.

- Mkuu wa Wilaya aliwaomba wananchi kujitokeza kwa wingi kwa kuwa maonesho haya hufanyika kikanda kila mwaka na kutoa fursa ya mkoa mmoja kuandaa maonesho. Hivyo, kuna kila sababu ya wananchi kufika katika mabanda kupata huduma za kibiashara na fedha kutoka kwa washiriki.

Mkuu wa Wilaya alihitimisha kwa kusema kuwa maonesho hayo yaliyoanza 21 Mei, 2023 yanatarajiwa kufungwa 27 Mei, 2023 na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma ambaye pia alimwakilisha Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (Mb.). Baada ya kusema hayo, Mkuu wa Wilaya aliyafungua rasmi maonesho ya sita ya mifuko na programu za uwezeshaji.

## 2.2 UFUNGAJI NA HOTUBA YA MGENI RASMI KUHITIMISHA KILELE CHA MAONESHO

### 2.2.1 UTAMBULISHO NA MADHUMUNI YA MAONESHO

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji **Bibi Beng'i Issa** pamoja na mambo mengine alianza kwa kumshukuru Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Kamishna Jenerali Mstaafu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mhe. Thobias Andengenye kwa kukubali kuwa mgeni rasmi wa maonesho ya sita ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Pia alimshukuru Mkuu wa Mkoa wa Tabora Dkt. Batilda Buriani Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Makatibu Tawala, wakuu wa taasisi za Umma na Binafsi, wadhamini viongozi kamati ya ulinzi na usalama, dini, washiriki, wajasiriamali, wananchi na waandishi wa habari. Maonesho yamehudhuriwa na jumla ya wananchi **12,673** ambapo wanawake ni **49%** ikilinganishwa na wanaume ambao walikuwa **51%,** idadi ya taasisi wezeshi **73** **i**kijumuisha waratibu wa madawati ya uwezeshaji ngazi ya mikoa **4** na waratibu ngazi ya halmashauri **26.** Sanjari na hayo, pia jumla ya wajasiriamali **185** wanawake ni **58%** na wanaume **52%**. Katibu Mtendaji pamoja na mambo mengine aliainisha mambo ya msingi yafuatayo:

- Ushiriki hafifu wa wananchi uliotokana na vikwazo vya kiuchumi kabla ya uhuru. Baada ya Uhuru mwaka 1961, wananchi walipata madaraka ya kisiasa lakini sehemu kubwa ya uchumi bado ilibaki mikononi mwa wageni na wananchi wachache. Kutokana na hali hiyo, Serikali ilitangaza Azimio la Arusha mwaka 1967 na kuanza utekekezaji wake lakini bado hali ya ushiriki wa ulikuwa mdogo kutokana na ukosefu wa mitaji; ukosefu wa ujuzi na uzoefu katika elimu; ukosefu wa dhamana ya mikopo; ukosefu wa masoko ya uhakika au uwezo wa kuingia katika masoko yenye ushindani.

- Mwaka 1983 Serikali ilianzisha mifuko na programu za uwezeshaji ambapo hadi kufikia Machi, 2023, kulikuwa na jumla ya mifuko na programu za uwezeshaji **73** ambazo zinatoa huduma za mikopo, dhamana na ruzuku kwa wananchi. Mifuko na proramu **63** zipo katika sekta ya Umma na **10** zipo katika taasisi za sekta binafsi. Kati ya mifuko na programu **73** zilizopo, mifuko **23** inatoa mikopo moja kwa moja, mifuko **11** inatoa dhamana, mifuko **28** inatoa ruzuku na **10** ni programu za uwezeshaji.

- Maonesho hufanyika kikanda na kwa mara ya **kwanza** yalifanyika mwaka 2017 katika Kanda ya Kati iliyohusisha mikoa ya Dodoma, Singida na Tabora; Maonesho ya **Pili,** yalifanyika Mbeya mwaka 2018 katika Kanda ya Nyanda za Juu yakihusisha mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, Rukwa, Ruvuma na Songwe; Maonesho ya **Tatu,** yalifanyika Simiyu Mwaka 2019 katika Kanda ya Ziwa na kuhusisha mikoa ya Geita, Kagera, Mara, Mwanza, Simiyu na Shinyanga na Maonesho ya **Nne,** yalifanyika Arusha mwaka 2021 katika Kanda ya Kaskazini na kuhusisha mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga. Maonesho ya **Tano,** yalifanyika Morogoro mwaka 2022 katika Kanda ya Mashariki na kuhusisha mikoa ya Dar Es Salaam, Pwani, Morogoro, Lindi na Mtwara, na Maonesho ya **Sita** yamefanyika Kigoma kwa kanda ya Magharibi na kuhusisha Mikoa ya Kigoma na Katavi.

Aidha, Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa lengo la kujenga uchumi jumuishi unaopunguza mzunguko wa umaskini kwa wananchi. Jitihada hizo ni pamoja na:

(i) Kuanzisha mifuko na programu za uwezeshaji kwa lengo la kutoa mikopo na dhamana ya mikopo kwa wananchi kwa masharti nafuu.

(ii) Hadi Machi, 2023, mifuko imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi **Trioni 6.1** kwa wajasiriamali **8,650,257** wakiwemo wanawake **4,747,321** na wanaume **3,902,936**. Aidha, mifuko na programu hizi zimetengeneza jumla ya ajira **17,603,271** ambapo ajira kwa wanawake zilikuwa **9,248,916** (**52.5%)** na wanaume ni **8,354,355** (**47.5%**)**.**

(iii) Jitihada nyingine ambazo zimechukuliwa na Serikali katika kuwawezesha wananchi kwenye shughuli za kiuchumi na kupunguza mzunguko wa umaskini ni pamoja na:

- Kutekeleza Mpango wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na vya Kati *(SANVN Viwanda Scheme)* kwa lengo la kutoa fursa kwa Watanzania kupata mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo na vya kati hususan vilivyochakata mazao ya kilimo na mifugo. Mpango umetoa mikopo yenye jumla ya thamani ya **Shilingi 3,619,896,907** kwa **miradi 63** iliyofanyika katika **mikoa 13**. Mikoa hiyo ni pamoja na: **Mwanza Arusha; Dar Es Salaam; Kilimanjaro; Mbeya; Geita; Dodoma; Shinyanga ; Iringa; Njombe; Singida; Pwani na Rukwa.**

- Kuanzisha vituo vya uwezeshaji kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 **Ibara ya 26 (K)** ili kuwezesha upatikanaji wa huduma uwezeshaji wananchi kiuchumi ambazo ni mikopo, mafunzo, urasimishaji wa biashara, ujuzi wa wafanyabiashara, uongezaji thamani ya mazao, elimu ya kodi na upatikanaji wa masoko. Hadi Machi, 2023 jumla ya vituo vya uwezeshaji **20** vimeanzishwa katika mikoa nane ya Shinyanga **(2),** Geita **(1),** Singida **(1),** Pwani **(1),** Morogoro **(1),** Rukwa – Sumbawanga **(1),**

Kigoma **(6)** na Dodoma **(7).** Vituo hivi viliwezesha upatikanaji wa mikopo yenye thamani ya **shilingi bilioni 9.4** kwa **wajasiriamali 4,017.**

Pamoja na jitihada hizo, bado kuna changamoto za jumla zinazokabili uwezeshaji wananchi na kusababisha mzunguko wa umaskini katika jamii. Changamoto hizo ni pamoja na:-

a) Kiwango kidogo cha upatikanaji wa huduma za fedha katika maeneo ya pembezoni na vijijini. Hali hii inakwamisha wafanyabiashara waliowekeza maeneo ya pembezoni na vijijini kushindwa kupanua biashara na wananchi kushindwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi.
b) Ukosefu wa mitaji kwa wananchi wanaohitaji kuanzisha au kukuza biashara kutokana na ukosefu wa dhamana.
c) Gharama kubwa ya upatikanaji wa huduma za fedha kutokana na riba kubwa na kufanya gharama kubwa za upatikanaji wa mikopo.
d) Kutorejeshwa kwa mikopo hasa inayotolewa na Mfuko wa Kuwawezesha Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kupitia asilimia 10 za mapato ya ndani ya Halmashauri.
e) Ukosefu wa dhamana kwa wananchi wakiwemo wajasiriamali wadogo na wa kati kutokana na eneo kubwa la ardhi nchini kutopimwa au kurasimishwa.

Hivyo, Baraza litaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuendelea kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanafikiwa na fursa mbalimbali za uwezeshaji nchini. Maonesho yalilenga kuleta matokeo chanya ikiwa ni pamoja na kukuza uelewa wa wananchi kuhusu kuwepo kwa mifuko na programu za uwezeshaji; kuwajenga utamaduni kwa wananchi wa kuweka akiba na kuwekeza katika miradi ya kiuchumi yenye kuleta faida; na kuongeza hamasa kwa mabenki ili wananchi wakopesheke kwa kutumia ardhi kama dhamana na kuhamasisha wananchi kujiunga kwenye vikundi vya kiuchumi kama SACCOS na VICOBA.

### 2.2.2 SALAAMU ZA MWENYEKITI WA BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI

Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi **Prof. Aureria Kamuzora** alianza kwa kuwashukuru viongozi, washiriki na wananchi kwa kujitokeza kwa wingi kushiriki kilele cha maonesho. Mwenyekiti katika salaam zake pamoja na mambo mengine alisisitiza mambo ya msingi yafuatayo:

- Umuhimu wa kuwa na mifumo ya kidigitali ili kuwezesha kubadilishana taarifa sahihi kwa wakati sahihi.
- Kujenga uchumi shirikishi wenye kushirikisha wananchi kunufaika na fursa za
- Kuendelea kutekeleza maelekezo ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) aliyoyatoa mwezi Aprili, 2017 ambapo pamoja na mambo mengine aliagiza kila mwaka maonesho yafanyike kikanda ili kuwafikia wananchi walio wengi hususani wale wa vijijini na kuwawezesha kutambua fursa za mifuko na programu za uwezeshaji
- Mwenyekiti wa NEEC alihitimisha kwa kumshukuru mgeni rasmi, viongozi, washiriki na wananchi kwa kujitokeza.

### 2.2 3 SALAAMU ZA MKOA WA KIGOMA

Salaamu za Mkoa wa Kigoma zilitolewa na Katibu Tawala wa Mkoa **Bw. Frank Charles** ambaye alianza kwa kuwashukuru viongozi wote kutoka Kigoma kwa ushirikiano wa kuratibu na kushiriki katika maonesho. Katika hizo salaam aliwashukuru viongozi ikiwa ni pamoja na mgeni rasmi, viongozi wa mikoa, wilaya, wajumbe wa kamati za ulinzi na usalama, washiriki, wajasiamali, vyombo vya habari. Aidha, RAS alitoa shukrani za dhati za kuushukuru uongozi mzima wa NEEC na Wizara kwa kuyaleta maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji mkoani Kigoma ambapo wananchi wameshiriki na kujifunza mengi ikiwa ni pamoja na kuainisha fursa mbalimbali kama vile masoko, mitaji, teknolojia na mafunzo. RAS pia aliwashukuru viongozi wote wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora Mhe. Balozi Dkt. Batilda Buriani, makatibu tawala wa mikoa ya Tabora, Katavi na Geita, viongozi na wawakilishi wa taasisi, asasi za kiraia, taasisi za elimu na utafiti, wafanyabishara, vikundi vya ujasiriamali, waratibu wa madawati ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Baada ya kuwasilisha salaam, Katibu Tawala alimkaribisha Mkuu wa Mkoa wa Tabora kutoa salaam kabla ya kumkaribisha Mgeni Rasmi ambaye alikuwa Mkuu wa Kigoma kuwasilisha hotuba.

### 2.2.4 SALAAMU ZA MKUU WA MKOA WA TABORA

Mkuu wa Mkoa wa Tabora **Mhe. Balozi Dkt. Batilda Salha Burian** alianza kwa kuishukuru serikali ya awamu ya tano kwa dhamira ya dhati ya kuendelea kuweka vipaumbele vya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Mkuu wa Mkoa aliwashukuru mwenyeji wake Mkuu wa Mkoa wa Kigoma pamoja na viongozi mbalimbali wa wizara, taasisi na washiriki kwa ujumla. Mkuu wa Mkoa wa Tabora katika salaam zake. Aidha, alikiri kuwa Mkoa wa Tabora umenufaika na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni **170**. Mkuu wa Mkoa alimshukuru Rais wa Awamu ya Sita Mhe. Dkt Samia Suluhu kwa maelekezo ya kuangalia utaratibu wa kuboresha na kuimarishwa mikopo ya **10%** ya mapato ya halmashauri zaidi ili kuongeza tija kubwa na ufanisi. Utaratibu huo unatarajiwa kuhusisha fedha kupitia mifumo ya mabenki ili kuongeza uwajibikaji na ufanisi wa utendaji kazi. Baada ya salaam, Mkuu wa Mkoa wa Tabora alimkaribisha Mgeni Rasmi Kamishna Mstaafu wa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji Mhe. Thobias Andengenye kuwasilisha hotuba ya mgeni rasmi na ufungaji wa kilele cha maonesho.

### 2.2.5 HOTUBA YA MGENI RASMI KUFUNGA KILELE CHA MAONESHO

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Kamishna Mstaafu wa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji **Mhe. Thobias Andengenye** alianza kwa kutembelea mabanda na baada matembezi aliwasilisha hotuba ya ufunguzi na kufunga kilele cha maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Mgeni Rasmi alianza kwa kuwashukuru viongozi mbalimbali, washiriki na wananchi kwa kuacha majukumu yao na kukubali kushiriki katika Maonesho yenye lengo la kukuza uelewa wa wananchi kuhusu fursa zilizopo katika mifuko na programu za uwezeshaji. Mgeni Rasmi aliwashukuru vilevile viongozi wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Baraza la Taifa la Uwezeshaji kwa uratibu na pia kwa wakuu wa taasisi zinazosimamia mifuko na programu za uwezeshaji pamoja na taasisi mbalimbali kwa kushiriki katika Maonesho ya Sita ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji. Sambamba na hayo, mgeni rasmi aliwashukuru wadhamini wa maonesho na viongozi wa mikoa wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora Dkt. Batilda Buriani pamoja na wajasiriamali na wananchi wa Mkoa wa Kigoma kwa

kujitokeza kushiriki katika maonesho.



*Pembeni Kushoto Bw. Juma Ally, Afisa Miradi kutoka TaFF akitoa maelezo kwa Mgeni Rasmi, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Mhe. Thobias Andengenye wakati wa ufunguzi wa maonesho. Pembeni kushoto ni Katibu Mtendaji wa NEEC, Bibi. Beng'i Issa pamoja na viongozi wengine wa Chama na Serikali.*

Mgeni Rasmi katika hotuba yake alisema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina dhamira ya dhati ya kuweka mazingira wezeshi ili kuwezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo. Hii ni kutokana na maelekezo ya Ilani ya Chama cha Tawala (CCM) ya Mwaka 2020 chini ya Ibara ya **26 (a)** hadi **(e).** Katika hotuba yake Mgeni Rasmi pamoja na mambo mengine aliainisha manufaa ya jitihada za mifuko na programu za uwezeshaji kama ifuatavyo:

- ✓ Takwimu za Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi zinaonesha hadi kufikia Machi, 2023, mifuko na programu za uwezeshaji zimetoa mikopo na dhamana yenye thamani ya shilingi trilioni **6.1** kwa wajasiriamali **8,650,257** wakiwemo wanawake **4,747,321** sawa na asilimia **54.9** na wanaume **3,902,936** sawa na asilimia **55.1.**

- ✓ Mifuko na programu za uwezeshaji imetoa jumla ya ajira **17,603,371** ambapo ajira **9,248,916** ni wanawake sawa na asilimia **52.5** na ajira **8,354,355** ni wanaume sawa na asilimia **47.5.** Mikopo, dhamana na ruzuku zilitolewa katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, viwanda na biashara, utalii, misitu, sanaa, utamaduni na michezo.

- ✓ Mpango SANVN Viwanda Scheme umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni **3.62** katika miradi **63** ambayo imetolewa katika mikoa **13** ya Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza, Shinyanga, Geita, Dar es Salaam, Tabora, Songwe, Simiyu, Iringa, Arusha, Njombe na Dodoma. Mpango pia umetengeneza jumla ya ajira **3,384** huku ajira **697** (wanawake asilimia **56** na wanaume asilimia **44**) zikiwa za moja kwa moja na **2,687** zikiwa ni ajira zisizo za moja kwa moja katika Sekta za Kilimo, Mifugo, Ujenzi, Viwanda, Misitu na Maliasili. Mgeni Rasmi alitoa wito kwa wafanyabiashara kuendelea kutumia fursa za mikopo na dhamana kupitia

Mpango huu ili kutekeleza shughuli mbalimbali za kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, uvuvi na mifugo.

- ✓ Uzinduzi wa Programu ya *Building Better Tomorrow (BBT)* ambayo inalenga kuongeza ushiriki wa vijana katika kilimo kwa kupatiwa mafunzo, maeneo ya mashamba, mitaji na kuwaunganisha na fursa za masoko. Hadi Machi, 2023, jumla ya vijana **812** wameshiriki kwenye programu hiyo na kupawa ujuzi mbalimbali kwenye masuala ya kilimo.

- ✓ Uwepo wa vituo vya uwezeshaji ambavyo vinatoa huduma mbalimbali za mikopo, elimu ya ujasiriamali, teknolojia, masoko, alama za ubora na ithibati ya bidhaa, urasimishaji wa biashara, ukaguzi wa bidhaa, huduma za uandaaji wazo la biashara na huduma za uandaaji wa mpango wa biashara. Taarifa za NEEC zinaonesha hadi Machi, 2023, jumla ya vituo vya Uwezeshaji **20** vimeanzishwa katika mikoa nane **(20)** ya Shinyanga **(2),** Singida **(1),** Geita **(1),** Rukwa **(1),** Dodoma **(7),** Pwani **(1),** Morogoro **(1)** na Kigoma **(6).** Vituo vya uwezeshaji vimetoa huduma kwa wananchi **34,441** (wanaume **21,646** na wanawake **12,795**). Vituo vimewezesha upatikanaji wa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni **9.4** kwa wajasiriamali **4,017.**

Aidha, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) imeonesha kuwa, utendaji wa baadhi ya mifuko na programu za uwezeshaji kutokufanya vizuri hali iliyochangiwa na uwepo wa kiwango kikubwa cha mikopo chechefu; utoaji wa mikopo kwa vikundi hewa; utoaji wa mikopo isiyokidhi malengo ya wakopaji na hivyo kutumia fedha walizokopa kwa matumizi mengine; baadhi ya mifuko na programu kutotekeleza malengo yaliyokusudiwa; utozaji wa riba kubwa kwenye mikopo; kutokuwa na mkakati endelevu wa marejesho ya mikopo; na matumizi mabaya ya fedha za mifuko na programu za uwezeshaji.

Hivyo, kutokana na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mgeni rasmi alisisitiza na kuwaomba maafisa masuuli na watendaji wakuu wa mifuko na programu za uwezeshaji kuyafanyia kazi masuala yafuatayo:

(i) Mikopo itolewa kwa mtu, kampuni au vikundi hai ambavyo vina biashara endelevu ili kuondoa tatizo la mikopo chechefu na vikundi hewa;

(ii) Kuhakikisha kiwango cha mikopo kinatolewa kulingana na mahitaji halisi ya kuanzisha au kuendeleza biashara. Kuhakikisha pia riba za mabenki na mifuko zinapunguzwa na kufikia *single digit* ili kupunguza gharama za biashara;

(iii) Wafanyabiashara watumie vyema mikopo na kufanya marejesho kwa wakati ili kujenga mahusiano mazuri na taasisi zinazosimamia mifuko na programu za uwezeshaji na taasisi za fedha;

(iv) Wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa nchini kuzalisha bidhaa bora zenye kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa ili kujenga uwezo wa kiushindani katika masoko ya ndani, ya kikanda na kimataifa pamoja na kuongeza matumizi ya kidigitali;

(v) Wananchi wanaopokea ruzuku kuhakikisha zinatumika kwenye malengo yaliyokusudiwa ili kupunguza umaskini wa kipato na mzunguko wa umaskini katika jamii.

Baada ya hotuba ya mgeni rasmi, hafla ya utoaji wa mikopo ya *SELF Microfaince* na *SANVN Viwanda Scheme* kwa wanufaika pamoja na zoezi la utoaji wa tuzo kwa taasisi ambazo zilishinda kutokana na kufanya vizuri katika maonesho yalikuwa kama ifuatavyo:

#### 2.2.5.1 Mikopo Wakati wa Maonesho

Mgeni Rasmi ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Kigoma kukabidhi kwa hundi (Dummy Cheque) ya mikopo iliyotolewa yenye thamani ya shilingi **315,000,000/=** kwa wajasiriamali wawili walionufaika na fursa za mikopo kutoka SELF MF na Mpango wa SANVN viwanda scheme. Mgeni Rasmi alikabidhi hundi kiasi cha shilingi **140,000,000/=** iliyotolewa na SELF Microfinance kwa kampuni ya *Ihacha Credit Microfinance* iliyopo mkoani Kigoma. Sambamba na hayo, mgeni rasmi alikabidhi pia hundi yenye thamani ya shilingi **175,000,000/=** iliyotolewa na Mpango wa SANVN kwa kampuni ya *B&L Agridigital* iliyopo Dar es Salaam ambayo inayojishughulisha na utengenezaji wa mafuta ya kupikia ya alizeti. Sambamba na hayo, mgeni rasmi alitoa rai pia kwa watendaji wa kata na vijiji kuendelea kutoa ruzuku kwa kaya maskini ili zinufaike na fursa mbalimbali ikiwemo mfuko wa jamii wa TASAF.

#### 2.2.5.2 Utoaji wa Tuzo za Washindi

Tuzo mbalimbali za makundi zilitolewa kwa washindi wa makundi na Mgeni Rasmi katika kilele cha maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji kwa kuzingatia masharti na vigezo vilivyowekwa. Tuzo ziliainishwa katika makundi **Saba (7)** yaliyojumuisha taasisi 43, Halmashauri 26 na Wajasiriamali 185 walioshindanishwa katika kila kundi. Kila mshindi alipewa ngao na cheti cha ushindi. Zoezi la kuwapata washindi wa tuzo liliendeshwa na majaji huru kwa kuzingatia vigezo vilivyainishwa na Kamati ya Tuzo. Tuzo zilitolewa katika *taasisi ya fedha; halmashauri; taasisi za serikali; mifuko na programu za uwezeshaji; wajasiriamali; vyuo vya elimu na elimu ya juu; na wadhamini*. Vigezo vilivyotumika kupima na kuwapata washindi katika makundi ni pamoja na *huduma kwa wateja; ubunifu; muonekano wa watoa huduma; muonekano na mpangilio wa banda; na kujali muda na kufuata ratiba.*

**Jedwali Na. 2: Washindi wa Tuzo kwa Makundi**

| Na | Kundi la Tuzo | Idadi ya Taasisi zilizoshindanishwa | Jina la Taasisi Iliyopata Tuzo ya Ushindi | Mshindi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | **Sekta ya Fedha (Mabenki)** | 5 | CRDB Bank Plc | Na. 1 |
| | | | Azania Bank | Na. 2 |
| 2. | **Mifuko na Programu za Uwezeshaji** | 11 | PASS TRUST Fund | Na. 1 |
| | | | UCSAF | Na. 2 |
| | | | SELF Microfinance | Na. 3 |
| 3. | **Taasisi za Umma** | | Wakala wa Vipimo (WMA) | Na. 1 |
| | | | TAKUKURU | Na. 2 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 25 | Hifadhi ya Gombe (Gombe Game Reserve) | Na. 3 |
| 4 | **Halmashauri** | 26 | Kibondo DC | Na. 1 |
| | | | Shinyanga MC | Na. 2 |
| | | | Kigoma Ujiji MC | Na. 3 |
| 5. | **Vyuo vya Elimu** | 6 | TIA | Na. 1 |
| | | | VETA | Na. 2 |
| | | | IFM | Na. 3 |
| 6. | **Wajasiriamali** | 185 | Serengeti Cultural Centre | Na. 1 |
| | | | Hadija Matiko | Na. 2 |
| | | | Aika Tery | Na. 3 |
| 7. | **Wadhamini** | 31 | TASAF | Na. 1 |
| | | | UCSAF | Na. 2 |

Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Mkoani Kigoma: NEEC (2023)**

### 2.2.6 NENO LA SHUKRANI KUTOKA WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA

Neno la shukrani lilitolewa na Bw. Condrad Milinga Mkurugenzi wa Uwezeshaji na Maendeleo ya Sekta Binafsi ambaye alimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ambaye hakuweza kushiriki kutokana na ratiba za shughuli nyingine za kitaifa kuingiliana. Katika salaam zake, Mkurugenzi alimshukuru Mgeni Rasmi Mkuu wa Mkoa wa Kigoma kwa kushiriki kama mwenyeji na pia ni heshima kubwa kwa Mkuu wa Mkoa kushiriki na kufunga kilele cha maonesho ya sita ya mifuko na programu za uwezeshaji.

Sambamba na hayo, akiwakilisha salaam za Wizara Mkurugenzi alitoa udhuru wa viongozi waandamizi wa wizara ambao ni Waziri mwenye dhamana na Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Naibu wake kutokana na ratiba kuingiliana na shughuli za Bunge. Hivyo, wizara ikawakilishwa na Mkurugenzi wa Uwezeshaji na Maendeleo ya Sekta Binafsi. Wizara pia imeshirikiana na NEEC kuratibu maonesho. Mkurugenzi katika salaam za wizara alisema;
.

- Wizara ipo katika utekelezaji wa maagizo na maelekezo ya Serikali kutembelea mikoa kubaini changamoto za wafanyabiashara nchini na kuzitafutia ufumbuzi wa namna ya kuzitatua.
- Wizara ya Uwekezaji Viwanda na Biashara kupitia NEEC itaendelea kuratibu na kusimamia shughuli za mifuko na programu za uwezeshaji ili kuwafikia wananchi walio wengi.

Mkurugenzi alihitimisha salaam zake kwa kumshukuru mgeni rasmi na kuyafuatilia yale yote aliyosisitiza ili kuendelea kuboresha na kuyafanya maonesho kuwa na tija kwa wananchi ambao ndio walengwa pamoja na taasisi zinazotekeleza uwezeshaji. Aidha, aliwashuru viongozi mbalimbali wa wizara, mikoa, taasisi na dini waliojitokeza kufunga kilele cha maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji.

## SURA YA TATU

## 3. MATOKEO YA TATHMINI YA MAONESHO YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI

Sehemu hii inaonesha tathmini ya uchambuzi wa taarifa za maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi mkoani Kigoma. hii imefanyika kwa washiriki wa maonesho ambao ni wajasiriamali**,** taasisi wezeshi za utoaji wa huduma za biashara (BDS Providers) na mifuko na programu za uwezeshaji. Matokeo ya tathmini ya wiki ya maonesho ya programu na mifuko ya uwezeshaji yamechambuliwa kama ifuatavyo:

### 3.1 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA TAARIFA ZA MAHUDHURIO

Matokeo ya uchambuzi wa tathmini ya mahudhurio ya wananchi, wajasiriamali, taasisi, watoa huduma za biashara na waratibu wa madawati ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ni kama ifuatavyo:

#### 3.1.1 MCHANGANUO WA MAHUDHURIO YA WANANCHI NA WASHIRIKI WA MAONESHO

Jumla ya washiriki na wananchi **12,673** huku wanawake wakiwa ni **6,193** na wanaume **6,480.** Sanjari na hayo, mgawanyo wa mahudhurio pia unaonesha wananchi walikuwa **12,167 (**wanawake **5,895** na wanaume **6,272**).

**Jedwali Na 3: Machanganuo wa Mahudhurio ya Wananchi na Washiriki wa Maonesho**

<table>
<tr><th rowspan="2">Na.</th><th rowspan="2" colspan="2">Kundi la Washiriki</th><th rowspan="2">Idadi ya Taasisi</th><th colspan="3">Idadi ya Washiriki katika Mabanda</th></tr>
<tr><th>Ke</th><th>Me</th><th>Jumla</th></tr>
<tr><td>1</td><td colspan="2">Mifuko na Programu za Uwezeshaji</td><td>24</td><td>141</td><td>91</td><td>232</td></tr>
<tr><td>3</td><td colspan="2">Watoa Huduma za Biashara (BDSP)</td><td>19</td><td>31</td><td>28</td><td>59</td></tr>
<tr><td rowspan="2">4</td><td rowspan="2">Waratibu wa Madawati ya Uwezeshaji</td><td>RECO</td><td>4</td><td>2</td><td>2</td><td>4</td></tr>
<tr><td>DECO</td><td>26</td><td>21</td><td>5</td><td>26</td></tr>
<tr><td>5</td><td colspan="2">Wajasiriamali</td><td>-</td><td>108</td><td>77</td><td>185</td></tr>
<tr><td>6</td><td colspan="2">Wananchi</td><td>-</td><td>5,895</td><td>6,272</td><td>12,167</td></tr>
<tr><td colspan="3">Jumla</td><td>73</td><td>6,193</td><td>6,480</td><td>12,673</td></tr>
</table>

Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Mkoani Kigoma: NEEC (2023)**

Aidha, ushiriki katika jinsi unaonesha wanaume walikuwa ni **6,480** sawa na 51% ya wananchi pamoja na washiriki **12,673** ikilinganishwa na wanawake **6,193** sawa na 49%. Tathmini pia imebaini kuna haja ya kuwa na mkakati utakaohakikisha taasisi za sekta binafsi, taasisi za utafiti, asasi za kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na miamvuli (umbrellars – promoters) wa vikundi vya kifedha vya kijamii ili kutoa elimu kwa umma pamoja na kuonesha jitihada za uwezeshaji zilizofanyika na taasisi wezeshi. Makundi hayo ni muhimu ili kuwezesha wananchi kutambua na kuainisha fursa za uwezeshaji kupitia sekta mbalimbali za kiuchumi.

#### 3.1.1.1 Idadi ya Wajasiriamali na Taasisi za Utoaji Huduma za Biashara na Fedha

Maonesho yalihudhuriwa na jumla ya wajasiriamali **185** (wanawake **108** na wanaume **77**) na washiriki wa programu na mifuko ya uwezeshaji **232** (wanawake **141** na wanaume **91**) na watoa huduma za biashara (BDSP) **59** huku wanawake wakiwa **31** na wanaume **28** kutoka katika taasisi **43** huku za umma zikiwa ni **28** na kutoka sekta binafsi **15** zilizoshiriki maonesho.


#### 3.1.1.2 Idadi ya Waratibu wa Madawati ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Matokeo ya uchambuzi yanaonesha maonesho yalihudhuriwa na waratibu wa madawati ya uwezeshaji **30** (wanawake **23** na wanaume **7**) ambao ngazi ya mikoa walikuwa ni wanne (**4**) kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Geita, Kilimanjaro na Kigoma na waratibu wa madawati ya uwezeshaji **26** kutoka Halmashauri za *Arusha CC, Dar es salaam CC, Mwanza CC, Kahama MC, Kinondoni MC, Bukoba MC, Songea MC, Ifakara TC, Njombe TC, Muleba DC, Buchosya DC, Hai DC, Bukoba DC, Arusha DC, Mlele DC, Kibaha DC, Itilima DC, Nyasa DC, Igunga DC, Misungwi DC, Biharamulo DC, Maswa DC, Misenyi DC, Bariadi DC, Nsalala DC,* na *Ushetu DC*. Maonesho pia yalihudhuriwa viongozi mbalimbali kutoka katika wizara, mikoa, wilaya, halmashauri, wakuu wa taasisi za Umma na Binafsi na vyama vya siasa. Jedwali hapa chini linaonesha mchanganuo wa makundi ya washiriki wa wiki ya mifuko na programu za uwezeshaji.

#### 3.1.1.3 Idadi ya Washiriki *Exhibotors* Katika Mabanda

Tathmini inaonesho maonesho yalihudhuriwa na jumla ya washiriki waoneshaji (exhibitors) **258** ambapo jinsi ya wanawake ilikuwa ni **191** sawa na **74%** ikilinganishwa na wanaume ambao walikuwa ni **67** sawa na **26%** kama mchoro hapa chini unavyoonesha. Idadi ndogo ya ushiriki wa wanaume unatokana na mwamko mdogo wa wanaume kujiunga katika vikundi vya uzalishaji mali na kujishughulisha bidhaa za uongezaji thamani ambapo wanawake wanaonekana kufanya vizuri. Hivyo, bado hamasa inahitajika kutolewa ili kuwezesha uwepo wa uwiano mfanano wa jinsi katika ushiriki wa maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa mwaka 2024.

**Mchoro Na. 1: Idadi ya Washiriki Waoneshaji wa Maonesho katika Mabanda**





Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Mkoani Kigoma: NEEC (2023)**

### 3.1.1.4 Idadi ya Wananchi Waliohudumiwa Katika Mabanda

Wananchi wameonesha hamasa kubwa ya kushiriki maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji. Matokeo ya tathmini yanaonesho jumla ya wananchi **12,167** walihudumiwa katika mabanda ya washiriki wa maonesho kwa siku nane. Mgawanyo wa jinsi unaonesha wanaume **6,272** sawa na **52%** ikilinganishwa na wanawake **5,895** ambao walikuwa ni **48%.** Idadi kubwa ya wanaume kutembelea mabanda imetokana na hamasa ya mifuko na programu za uwezeshaji kuwa na matokeo chanya katika kuwadumia wateja pamoja na fursa nyingine za ubunifu, utoaji wa huduma za biashara. Vilevile, tathmini inaonesha ongezeko la wananchi katika siku ya kwanza hadi siku ya tano huku wanawake wakionekana kuwa wengi siku ya nne wakati pia siku ya saba na nane mahudhurio yalizidi zaidi kama mchoro unavyoonesha hapa chini.

**Mchoro Na. 2: Idadi ya Wananchi Waliohudumiwa Katika Mabanda**




| | Siku ya 1 | Siku ya 2 | Siku ya 3 | Siku ya 4 | Siku ya 5 | Siku ya 6 | Siku ya 7 | Siku ya 8 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 388 | 514 | 722 | 584 | 957 | 803 | 1102 | 1202 |
| Wanawake | 401 | 467 | 651 | 720 | 801 | 710 | 1018 | 1127 |

Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Mkoani Kgoma: NEEC 2023**

## 3.2 MATOKEO YA TATHMINI YA MAKUNDI YA WASHIRIKI WA MAONESHO

Matokeo ya tathmini ya maonesho ya mifuko na programu za uweshaji yameainishwa kwa kuzingatia uchambuzi uliofanyika kwa wajasiriamali, watoa huduma za biashara na mifuko ya uwezeshaji kama ifuatavyo:

### 3.2.1 WAJASIRIAMALI


### 3.2.1.1 Taarifa za Ushiriki kwa Wajasiriamali Katika Maonesho

Tathmini yalibaini vyanzo mbalimbali vya vilivyosaidia wananchi kupata taarifa za maonesho kuwafikia walengwa kwa wakati. Matokeo ya tathmini yaliyofanywa kwa wajasiriamali **112** kati ya **185** walioshiriki maonesho. Matokeo yanaonesha wajasiriamali **45** sawa na **61%** ya wajasiriamali **112** waliohojiwa walikiri kuwa vyombo vya habari viliwezesha kupata taarifa za maonesho kwa wakati sahihi. Katika kuwafikia wananchi, televisheni ilionekana kuongoza huku wajasiriamali **27** wakiriki na kufuatiwa na redio

ambapo wajasiriamali **10** ya waliohojiwa walikiri kupitia chombo cha habari cha redio huku wajasiriamali **8** wakiainisha kupitia magazeti.

Sanjari na hayo, wajasiriamali **23** waliainisha mitandao ya kijamii kama vile *tweeter* **(5),** *instagram* **(8),** *facebook* **(11)** imechangia kupata taarifa huku wajasiriamali 19 wakibainisha walipata taarifa kupitia matangazo ya barabarani. Aidha, tathmini pia ilibaini wajasiriamali **17** walipata taarifa za maonesho kupitia Halmashauri za Wilaya kupitia waratibu wa madawati ya uwezeshaji wananchi kiuchumi wakati wajasiriamali **8** waliainisha vyanzo vingine ambavyo ni marafiki, vikundi vya kifedha vya kijamii.

**Mchoro Na. 3: Vyanzo vya Taarifa za Maonesho**




Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Mkoani Kigoma: NEEC (2023)**


Pamoja na hayo, tathmini ilibaini kuwa wananchi **69** waliohojiwa wamekiri umuhimu wa kuwashirikisha viongozi wa dini ambao pia ni wajumbe wanaounda kamati za ulinzi na usalama za mikoa. Ushirikishwaji wa viongozi wa dini unaonekana kuwa manufaa mengi katika kufikisha ujumbe na kushawishi waamini kuhudhuria na kushiriki maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji ambazo hufanyika mara moja kila mwaka. Matangazo ya mwezi mmoja kabla ya maonesho katika makanisa na misikitini yataongeza ushiriki wa idadi kubwa ya wananchi kupata taarifa na pia kufahamu jitihada na juhudi za Serikali za uwezeshaji wananchi kiuchumi.

#### 3.2.1.2 Viwango vya Elimu vya Wajasiriamali

Tathmini ilibainisha jinsi na viwango vya elimu vya wajasiriamali walioshiriki katika maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji kwa lengo la kujua aina ya washiriki, mapungufu pamoja na mahitaji ya mafunzo yaliyohitajika katika mafunzo ambayo yaliratibiwa na NEEC. Matokeo ya tathmini iliyofanyika yanaonesha kulikuwa na jumla ya washiriki wajasiriamali **185** ambapo kati yao wajasiriamali **112** walihojiwa kati yao wanaume ni **31** huku wanawake wakiwa ni **77** na walemavu ni **4** ambapo mwanaume alikuwa **1** huku wanawake wakiwa ni **3**. Idadi ya wanawake kushiriki inaonekana kuwa **89.6%** ikilinganishwa na wanaume ambao ni **10.4%** hii inatokana na hamasa ya

wanawake kuwa na uthubutu wa kufanya biashara unaochangiwa na uelewa kuongezeka wa kujiajiri kupitia sekta binafsi. Vilevile, ongezeko la wanawake katika maonesho linatokana na mafunzo ambayo yamekuwa yakitolewa bila gharama na kuratibiwa na NEEC kwa lengo la kukuza ubunifu, maarifa na ujuzi wa ujasiriamali katika kukuza mitandao ya kibiashara na masoko kwa ujumla wake.

**Mchoro Na. 4: Viwango vya Elimu vya Wajasiriamali**





Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Mkoani Kigoma: NEEC (2023)**

Sanjari na hayo, tathmini inaonesha uwepo wa viwango tofauti vya elimu kwa wajasiriamali walioshiriki maonesho. Mchoro hapa chini unaonyesha viwango vya elimu vya wajasiriamali **112** ambao walifanyiwa tathmini na matokeo kuonyesha kuwa hakuna mjasiriamali hata mmoja ambaye hakusoma shule. Matokeo ya tathmini yameonesha wajasiriamali **75** walihitimu elimu ya msingi, wahitimu wa elimu ya sekondari walikuwa **23** ambapo kati yao **85%** ya washiriki walikuwa na elimu ya kidato cha nne na **15%** walikuwa ni kidato cha sita. Kwa upande wa elimu ya vyuo kwa viwango vya cheti na diploma walikuwa wajasiriamali **6** na wale wenye elimu ya chuo kikuu walikuwa **8**. Sampuli ya washiriki waliohojiwa inaonyesha dhahiri kuwa idadi kubwa ya wajasiriamali wenye elimu ya shule ya msingi wamekuwa na ujasiri mkubwa wa kujishughulisha na shughuli za kiuchumi hususani katika nyanja ya kujiajiri na kutoa ajira kwa makundi mengine katika kufanya biashara ndogo ndogo na za kati.

Matokeo ya tathmini inaonyesha kuwa wajasiriamali wenye elimu ya msingi na sekondari pamoja na wale wa vyuo vya kati wamekuwa na mwamko wa kujiajiri na kufuatilia zaidi taarifa na fursa za mikopo, dhamana, ruzuku, mafunzo, teknolojia na masoko. Hivyo, ushiriki wa makundi haya umekuwa na tija kwa maendeleo ya biashara katika kujifunza na kuongeza ubunifu wa bidhaa zinazoingia masokoni. Kwa kufanya hivyo, maonesho haya yanadhihirisha umuhimu wa Serikali na wadau wa Sekta Binafsi kuendelea kutoa kipaumbele ili kuongeza tija ya maonesho haya katika kuwafikia wananchi walio wengi kufahamu jitihada na juhudi za uratibu wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi kila mwaka**.**

**Mchoro Na.5: Viwango vya Elimu vya Wajasiriamali**




Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Mkoani Kigoma: NEEC (2023)**

Tathmini pia ilipima aina za biashara ambazo wajasiriamali wanajishughulisha nazo ambapo matokeo yanaonesha kuwa **72%** ya biashara za wajasiriamali walioshiriki maonesho zipo katika kundi la biashara ndogo ndogo (micro enterprises) na **23%** ni biashara ndogo (small enterprises) huku **5%** zikiwa ni biashara za kati. Hivyo, uwezeshaji bado unaonekana kuwa na umuhimu wake katika kuwajengea uwezo na kuliendeleza kundi la wajasiriamali wadogo wadogo pamoja na lile la wajasiriamali wadogo ili wakue na kuchangia ukuaji wa uchumi wa taifa letu na hatimaye kuzalisha kwa wingi ajira kwa wananchi wa Tanzania.

### 3.2.1.3 Ujengaji Uwezo wa Mafunzo ya Urasimishaji kwa Wajasiriamali

Tathmini ya mafunzo ya ujasiriamali, urasimishaji na fursa za mitaji wakati wa maonesho inaonesha jumla ya wajasiriamali **185** huku wanawake wakiwa ni **133** ikilinganishwa na wanaume **52** walioshiriki maonesho walinufaika na mafunzo yaliyoratibiwa na NEEC kwa kanda ya magharibi Mkoani. Mafunzo yaliwakutanisha wataalam kutoka taasisi **nane (8)** za utoaji wa huduma za biashara (BDSP) na fedha ambazo ni OSHA, GS1 TZ, SIDO, BRELA, TBS, TRA, NSSF na Azania BANK. Mafunzo kwa wajasiriamali yalilenga kujenga uelewa wa pamoja kuhusu huduma mablimbali zitolewazo na taasisi wezeshi za masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Mafunzo pia yalilenga kuwaunganisha wajasiriamali na fursa za mafunzo, mikopo, dhamana, ruzuku na kufahamu taratibu na huduma za taasisi wezeshi. Mafunzo yamesaidia katika kukuza uelewa wa wajasiriamali kufahamu taratibu na huduma mbalimbali za urasimishaji wa biashara, kampuni ama vikundi katika mamlaka katika taasisi zinazotoa huduma za usajili na utoaji wa alama za msimbomilia (Bar-code), leseni za biashara (BRELA), alama za ubora (TBS), OSHA, Elimu ya Mlipa Kodi (TRA), Kujiunga na huduma za mifuko ya hifadhi (NSSF), na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA). Taasisi nyingine zilizowezesha mafunzo kwa wajasiriamali ni SIDO, NSSF, na TAKUKURU.

**Jedwali Na. 4: Idadi ya Wajasiriamali Walionufaika na Mafunzo ya Urasimishaji**

| Na. | Taasisi | Mada za Mafunzo | Idadi ya Wajasiriamali Idadi Idadu ya Wanufaika wa Mafunzo | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ke | Me | Jumla |
| **1.** | OSHA | Usalama Mahali pa Kazi | **17** | **6** | **23** |
| **2.** | SIDO | Fursa za Mafunzo, Uatamizi, Uendelezaji Viwanda, Mikopo na Dhamana kwa wajasiriamali | **16** | 7 | **23** |
| **3.** | GS1 TZ | Umuhimu wa Msimbo Milia (Bar-code) katika Biashara | **17** | 7 | **24** |
| **4.** | BRELA | Usajili na Umiliki wa Leseni na Biashara | **17** | 6 | **23** |
| **5.** | TBS | Alama za Ubora katika Biashara | **16** | 7 | **23** |
| **6.** | TRA | Elimu ya Mlipa Kodi na upatikanaji wa TIN na VAT | **17** | 6 | **23** |
| **7.** | NSSF | Uhamasishaji wa Wananchi kuhusu Fursa za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii | **17** | 6 | **23** |
| **8.** | Azania Bank | Fursa za Mikopo / SANVN | **16** | 7 | **23** |
| | | **Jumla** | **133** | **52** | **185** |

Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Mkoani Kigoma: NEEC (2023)**

Aidha, matokeo ya tathmini ya mafunzo yanaonyesha kuwa mafunzo haya yamekuwa na tija kwa wajasiriamali kufahamu huduma mbalimbali zitolewazo na taasisi husika za utoaji wa huduma wezeshi za biashara. Tathmini inaonyesha wajasiriamali **69** (**77.3%)** kati ya **112** wamekiri kuwa wamewahi kushiriki mafunzo ikilinganishwa na wajasiriamali **43** (**22.7%**) ambao hawakuwahi kuhudhuria wala kushiriki mafunzo yaliyowaleta taasisi za wezeshi za huduma za biashara pamoja. Tathmini vilevile imeainisha **93%** ya wajasiriamali waliohojiwa walikiri kuwa hawajashiriki mafunzo kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja hadi miaka miwili kutokana na gharama za mafunzo zinazoendeshwa na watoaji wa huduma kuwa kubwa. Sanjari na hayo, mrejesho wa mafunzo yaliyotolewa wakati wa maonesho unaonesha **87%** ya washiriki **112** waliohojiwa walinufaika na mafunzo na kukiri kuwa mafunzo yaliyotolewa yalikuwa mazuri huku **13%** hawakuridhika na mafunzo huku sababu kubwa ikiwa ni mazingira ya darasa hayakuwa rafiki na vitini vya mada hawakupatiwa na vilevile wawezeshaji hawakutumia vifaa vya mafunzo kama vile projector ambazo kwa namna moja ama nyingine huongeza utulivu wa washiriki wa mafunzo.

Hivyo, kutokana na maonesho haya kuna haja ya maonesho haya kuwa endelevu na pia elimu ya ujasiriamali kwa njia ya nadharia na vitendo iendelee kuhamasishwa kutolewa ili kujenga nidhamu ya biashara na ushindani wenye tija kwa wajasiriamali. Aidha, kuna hitaji la kuandaliwa kwa Mwongozo wa Taifa wa Watoaji wa Huduma za Biashara (BDS Providers) ili waweze kusajiliwa na kuratibiwa na NEEC katika utoaji wa

mafunzo yenye tija na kukidhi ithibati kwa wajasiriamali. Hivyo, inashauriwa mapungufu yaliyojitokeza wakati wa mafunzo yanapaswa kufanyiwa maboresho katika maonesho ya mwaka 2024. Jedwali hapa chini linaonesha matokeo ya tathmini iliyofanywa kwa wajasiriamali wanufaika wa mafunzo:

**Jedwali Na. 5: Matokeo ya Tathmini ya Mafunzo kwa Wajasiriamali**

| Na | Matokeo ya Tathmini ya Mafunzo kwa Wajasiriamali wa Maonesho | Matokeo ya Tathmini (%) | |
|---|---|---|---|
| | | Ndiyo | Hapana |
| 1. | Mafunzo kukidhi matarajio | 95 | 5 |
| 2. | Mjasiriamali kutumia maarifa ya mafunzo niliyojifunza | 83 | 7 |
| 3. | Malengo ya mafunzo kwa kila mada yaliainishwa na kuzingatiwa ipasavyo na wawezeshaji | 56 | 46 |
| 4. | Kuridhika na maudhui ya mafunzo yaliyotolewa | 71 | 29 |
| 5. | Mjasiriamali aliwezeshwa kupata vitini vya mada | 8 | 92 |
| 6. | Wawezeshaji walikuwa na maarifa na wenye weledi | 88 | 12 |
| 7. | Muda uliotolewa wa majadiliano ulijitosheleza | 46 | 54 |
| 8. | Muda wa mafunzo ulikuwa kutosha | 21 | 81 |
| 9. | Mazingira ya darasa la mafunzo yalikuwa mazuri | 87 | 13 |

Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Mkoani Kigoma: NEEC (2023)**

Matokeo ya tathmini ya mafunzo iliyofanyika kwa wajasiriamali wakati wa maonesho yamebaini na kupendekeza mambo mbalimbali ambayo yanapaswa kufanyiwa kazi. Miongoni mwa mapendekezo hayo ni pamoja na haya yafuatayo:

- Muda wa mafunzo ulikuwa mfupi ukilinganisha na maudhui ya mada za wawezeshaji. Hii ilichangia kwa wajasiriamali kuingia na kutoka kwa lengo la kuwahi mabandani. Wajasiriamali wanashauri utengwe muda maalum wa mafunzo kwa takribani siku mbili kabla ya maonesho kuanza ili maarifa waliyoyapata yaweze kuwasaidia kwa kina wakati na baada ya maonesho
- Wajasiriamali wanashauri kupatiwa vitini ili kuwezesha kujenga maarifa zaidi na kuwaelimisha wale ambao hawakuweza kushiriki. Vitini vya mada ni muhimu kutolewa kwa mjasiriamali ili kuwa na uendelevu wa maarifa na ujuzi utakaochangia urasimishaji wa biashara ndogo ndogo
- Muda wa majadiliano haukuwa rafiki na hivyo wajasiriamali kushindwa kuuliza maswali na kupata ufafanuzi wa kutosha. Aidha, ushirikishwaji wa wajasiriamali ulikuwa hafifu.


Pamoja na changamoto zilizoainishwa hapo juu, wajasiriamali walikiri kuwa mafunzo kwa **95%** yamekidhi matarajio kutokana na wawezeshaji kutoka katika taasisi wezeshi ambazo zimewezesha kuongeza uelewa wa usajili na urasimishaji wa biashara. Sanjari na hayo, **5%** ya waliohojiwa wanakiri kuwa mafunzo kutokukidhi matarajio kutokana na vipindi vya mafunzo kufanyika wakati wa maonesho na badala ilipendekezwa mafunzo yafanyike kabla ya maonesho kuanza.

#### 3.2.1.4 Aina za Biashara za Wajasiriamali na Ushiriki katika Mikoa

Maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji yamefanikiwa kuwaleta wajasiriamali wenye biashara za aina tofauti tofauti. Jumla ya wajasiriamali **185** ambapo wawili walitoka Bujumbura, Burundi na wengine kutoka katika mikoa ya Kigoma **(118),** Geita **(7), Mara (8),** Shinyanga **(13),** Tabora **(21),** Dodoma **(11),** Dar es Salaam **(5)** na kutoka Bujumbura Burundi **(2)** walifanikiwa kushiriki maonesho ambapo pamoja na mambo mengine wajasiriamali walifanikwa kuonesha bidhaa za sekta mbalimbali kama vile usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao, mbegu za mazao ya kilimo, ufugaji wa samaki na kuku, utengenezaji wa batiki na ushonaji wa nguo, vifaa vya ujenzi, ususi wa nyungo, ufumaji na ushonaji wa vikapu na mabegi, useketaji wa vikoi, sabuni za maji, dawa za asili, bidhaa na dawa za asili, Miche ya matunda, ubunifu wa mashine za uzalishaji, vifaa tiba vya hospitali, na pembejeo za kilimo. Matokeo ya tathmini yanaonyesha ushiriki wa wajasiriamali ulivyokuwa katika mikoa kama **jedwali** hapa chini linavyoonesha:

**Jedwali Na. 6 na Mchoro Na. 6: Idadi ya Wajasiriamali wa Maonesho Kimkoa**

| Nchi | Mkoa | Idadi ya Wajasiriamali | (%) |
|---|---|---|---|
| Tanzania na Burundi | Kigoma | 118 | 63.7 |
| | Tabora | 21 | 11.4 |
| | Shinyanga | 13 | 7 |
| | Dodoma | 11 | 6 |
| | Mara | 8 | 4.3 |
| | Geita | 7 | 3.8 |
| | Dar es Salaam | 5 | 2.7 |
| | Bujumbura | 2 | 1.1 |
| **Jumla** | | **185** | |




Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Mkoani Kigoma: NEEC (2023)**

Aidha, matokeo ya tathmini yanaonesha maonesho yalishirikisha jumla ya wajasiriamali **185** ambapo jinsi inaonesha kulikuwa na wanaume **52** sawa na **28%** ikilinganishwa na wanawake **133** ambao ni sawa na **72%.** Aidha, sampuli ya wajasiriamali **112** waliohojiwa inaonyesha **88%** ya wajasiramali hao wanajihusisha na biashara ndogo ndogo na wajasiriamali **10.3%** wakijihusisha na biashara ndogo huku biashara za kati zikiwa ni **2.7%**. Vigezo vilivyotumika kupima ni mtaji wa biashara na ajira ambazo biashara imeajiri pamoja urasimishaji wa biashara. Mbali na hayo, tathmini iliainisha aina ya biashara za wajasiriamali wanazojishughulisha nazo kama Jedwali hapa chini linavyoonesha.

**Jedwali Na. 7: Aina za Biashara Wajasiriamali**


| S/Na. | Aina za Biashara za Wajasiriamali | Idadi |
|---|---|---|
| 1. | Usindikaji wa vyakula na uongezaji thamani wa mazao | 44 |
| 2. | Miche na Pembejeo za kilimo | 36 |

| | | |
|---|---|---|
| **3.** | Utengenezaji samani – Useremala | 15 |
| **4.** | Useketaji, ufumaji na ushonaji wa vikapu, mabegi na ususi wa nyungo | 26 |
| **5.** | Mazao ya misitu na pembejeo za kilimo<br>Dawa/bidhaa za asili | 20 |
| **6.** | Sabuni za maji na uuzaji wa miche | 17 |
| **7.** | Ufugaji (Mf. Mbuzi, Kuku, Samaki n.k. | 8 |
| **8.** | Ubunifu wa mashine na vifaa vya Ujenzi | 19 |
| | **Jumla** | **185** |

Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Mkoani Kigoma: NEEC (2023)**

Tathmini ya maonesho imepima muda wa biashara za washiriki hususani wajasiriamali kwa nia ya kujua biashara zenye muda mfupi na zile ambazo zimekaa kwa muda mrefu pamoja na kutathmini hali halisi ya usajiri wa biashara katika mamlaka husika. Lengo pia kufahamu biashara mpya zilizoanzishwa, zile zenye uendelevu (survivalists) na zile zenye. Matokeo yanaonesha biashara zenye muda kati ya mwaka 1 hadi 3 ndizo zilizokuwa nyingi kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa huku tathmini ikibainisha zilikuwa **66,** zikifuatiwa na biashara zenye muda wa zaidi ya miaka 5 ambazo zilikuwa **32** na biashara zilizokuwa na muda wa zaidi ya miaka 3 hadi 5 zilikuwa **11** wakati zile zilizoanzishwa ndani ya mwaka mmoja zilikuwa **3** kama mchoro hapa chini unavyoonesha.

**Mchoro Na. 7: Muda wa Biashara za Wajasiriamali**





Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Mkoani Kigoma: NEEC (2023)**

### 3.2.1.5 Ushiriki wa Wajasiriamali, Usajili na Urasimishaji wa Biashara

Maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji yamekuwa na matokeo chanya katika kupima na kutathmini urasimishaji wa biashara na kujenga uelewa kwa wananchi kuhusu fursa za usajili wa biashara. Tathmini inaonesha kuwa maonesho ya mkoani

Kigoma yalihudhuriwa na wajasiramali **185** kutoka katika mikoa ya kigoma (**129**), Tabora (**21**), Shinyanga (**13**) na Geita (**7**), Dar es Salaam (**5**) Mara (**8**) na Burundi (**2**).

**Mchoro Na. 8: Ushiriki wa Wajasiriamali katika Mikoa**





Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Mkoani Kigoma: NEEC (2023)**

Aidha, sampuli ya wajasiriamali **122** ilifanyiwa tathmini ili kubaini hali halisi ya usajili kwa lengo la kufahamu urasimishaji wa biashara. Matokeo yanaonesha kuwa wajasiriamali **65** walifanikiwa kusajili biashara ikilinganishwa na wajasiriamali **57** ambao bado wanajishughulisha na biashara amabazo hazipo katika mfumo usio rasmi. Tathmini inaonesha **24%** ya wajasiriamali **65** waliofanikiwa kusajili biashara wanatoa risiti za mauzo ya bidhaa za biashara ikilinganishwa na **76%** ambao hawatoi risiti za ulipaji kodi.

Matokeo ya tathmini pia yanaonesha kuwa wajasiriamali **26** waliohojiwa walikiri kuwa wana namba za mlipa kodi huku wajasiriamali **76** wakiwa hawana namba hizo ambazo hutolewa bure na TRA. Mwenendo huu unaonesha bado elimu ya mlipa kodi inahitajika kuendelea kutolewa kwa wananchi wengi ili watambue umuhimu na wajibu wa kulipa kodi kwa maendeleo ya taifa. Kuna haja kuhamasisha pia taasisi wezeshi za usajili kutoa huduma katika mfumo wa pamoja (one stop centre) uliopo katika vituo vya uwezeshaji. Hii itachangia upatikanaji rahisi wa huduma na kuondoa usumbufu kwa wananchi kunufaika na fursa za huduma zitolewazo na taasisi wezeshi. Mchoro hapa chini unaonesha matokeo ya usajili wa biashara katika taasisi za BRELA, Halmashauri na nyingine kama GS1 TZ/SIDO

**Mchoro Na. 9: Biashara Rasmi na Zisizo Rasmi**




Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji, NEEC (2023)**

Matokeo yanaonesha kuwa biashara za wajasiriamali **33** kati ya **122** waliofanyiwa tathmini wamefanikiwa kupata alama ya ubora wa bidhaa inatolewa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ikilinganishwa na biashara **66** ambazo zilionekana kutokuwa na alama na alama huku sababu zikitajwa kutokuwa na uelewa wa kutosha unaochangiwa na elimu ndogo pamoja na gharama za upatikanaji wa alama za ubora wa bidhaa. Vilevile, tathmini ilihoji wajasiriamali kuhusu msimbomilia wa biashara. Wajasiriamali **25** walikiri kuwa biashara zao zina msimbomilia na zinatambulika na taasisi ya GS 1 TZ huku wajasiriamali **77** wakiwa hawana alama ya msimbomilia kutokana na kutoifahamu vizuri GS1 TZ licha ya SIDO kuwaunganisha wajasiriamali na fursa za upatikanaji wa huduma ya msimbomilia. Aidha, **68**% ya waliohojiwa walionekana kutofahamu taratibu za upatikanaji wa Namba ya Mlipa Kodi (TIN), Msimbomilia (Bar-code) ikilinganishwa na **32%** wenye ufahamu. Aidha, tathmini iliainisha kuwa usajili wa biashara kwa njia ya mtandao unachangia kuongeza gharama kubwa kwa wajasiriamali hususani wenye mitaji midogo ambao vilevile wana uelewa




mdogo wa TEHAMA na hivyo kulazimika kuwatumia watoa huduma za biashara (BDS Providers) katika usajili wa biashara.

Tathmini inapendekeza taasisi wezeshi zishirikishwe na kuweka wawakilishi katika vituo vya uwezeshaji ili kuwafikia wananchi na kutoa huduma stahiki. Uwepo wa taasisi kama vile *TRA, BRELA, TBS, GS1 TZ* katika vituo vya uwezeshaji utachochea wananchi hususani wajasiriamali kuingia katika mfumo ulio rasmi wa biashara na hatimaye kuongeza idadi ya walipaji wa kodi. Vituo vya uwezeshaji vianzishwe kwa wingi ili kuboresha maeneo ya huduma na kutoa elimu na mafunzo kwa wananchi. Hii itachangia upatikanaji rahisi wa mitaji yenye riba na masharti nafuu kwa wananchi wenye uhitaji wa mikopo inayopatikana hapa nchini.

#### 3.2.1.6 Vyanzo vya Mitaji ya Wajasiriamali

Matokeo ya tathmini yanaonesha vyanzo vya mitaji vilivyobainishwa ni pamoja na ile ya binafsi, ndugu, jamaa na marafiki, mikopo kutoka taasisi za fedha na mabenki, kikundi, na uwekezaji wa hisa au hati fungani. Mchoro hapa chini unaonesha matokeo ya tathmini ya chanzo cha mtaji kwa sampuli ya jumla ya wajasiriamali **112** walioshiriki maonesho ya mifuko ya uwezeshaji. Tathmini iliainisha wajasiriamali **35** walipata mitaji iliyotokana na kujiunga na vikundi vya kiuchumi, wajasiriamali **32** walikiri kuwa mitaji binafsi imechangia kuanzisha biashara na miradi ya kiuchumi huku wajasiriamali **23** wakiainisha kunufaika na mikopo inayotokana na mabenki kama vile NMB Bank Plc, CRDB Bank Plc, TADB na taasisi za fedha ikiwa ni pamoja na mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kama vile *SELF MF, PASS TRUST, NEDF,SCG, AGITF, Halmashauri (YDF, WDF)* wakati wajasiriamali **10** wakisema kuwa wameanzisha biashara kutokana na msaada wa ndugu, jamaa na marafiki na wajasiriamali **12** wakiainisha vyanzo vingine kama vile SACCOS, AMCOS, uwekezaji wa hisa, hati fungani katika taasisi za uwekezaji kama vile UTT AMIS ambapo wamekuwa wakinufaika na gawio.

**Mchoro Na. 10: Vyanzo vya Mitaji vya Wajasiriamali wa Maonesho**




Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji, NEEC (2023)**

Matokeo ya tathmini yanaonesha **58%** ya wajasiriamali **112** wamekopa zaidi ya mara mbili kwa lengo la kukuza mitaji ili kuwezesha ukuaji wa biashara pamoja na kufanikiwa kusajili biashara katika mamlaka za urasimishaji. Sanjari na hayo, matokeo yalionesha kuwa **42%** ya wajasirimali waliofanyiwa tathmini haikuwahi kukopa zaidi ya mkopo wa awali huku sababu zikitajwa kuwa ni uelewa mdogo wa wananchi kuhusu elimu ya mikopo, mikopo ya kilimo kuchelewa kutolewa kwa wakati.

Jedwali hapa chini linaonyesha matokeo ya tathmini kuhusu mtaji wa biashara hapo awali wakati wa uanzishwaji wa biashara hadi kufikia Mei, 2023 huku matokeo yakionesha **74%** ya wajasiriamali **112** hapo awali walikuwa wakijishughulisha na biashara ndogo sana (micro enterprises) ikilinganishwa 58% ya wajasiriamali hadi kufikia Mei, 2023 ambapo takwimu zikionyesha uwepo wa ukuaji wa biashara 18 ambazo zimekuwa ni biashara ndogo. Aidha, **25%** ya wajasiriamali hapo awali walijishughulisha na biashara ndogo (small enterprises) zenye mtaji wa kuanzia Tshs **5,000,000/=** hadi **200,000,000/=** ikilinganishwa na **38%** ya wajasirimali wenye biashara ndogo hadi kufikia Mei, 2023. Biashara za Kati zenye mtaji wa kuanzia Tshs **200,000,000/=** hadi **800,000,000/=** hapo zilikuwa ni **1%** ikilinganishwa na **3%** hadi kufikia Mei, 2023. Hii inatokana na uwepo wa fursa za mikopo ambayo inachangia uimarishaji na ukuaji wa biashara pamoja na urasimishaji wa biashara. Sanjari na hayo, **1%** ya wajasiriamali hadi kufikia Mei, 2023 wanajishughulisha na biashara kubwa zenye mtaji wa zaidi wa Tshs **800,000,000/=**

**Jedwali Na 8: Mtaji wa Biashara wa Hapo Awali na Hadi Mei, 2023**


| Aina ya Biashara | Mtaji Biashara | Mtaji wa Awali wa Biashara | Mtaji Hadi (Mei 2023) |
|---|---|---|---|
| Ndogo Sana | 0 - 5,000,000 | 83 | 65 |
| Ndogo | ≥ 5,000,000 - 200,000,000 | 28 | 42 |
| Kati | ≥ 200,000,000 - 800,000,000 | 1 | 4 |
| Kubwa | ≥ 800,000,000 | 0 | 1 |

Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji, NEEC (2023)**

### 3.2.1.7 Mikopo na Marejesho ya Wajasiriamali

Mchoro hapa chini unaonyesha matokeo ya tathmini ya muda wa marejesho ya mikopo kwa sampuli ya wajasiriamali **112** waliofanyiwa mahojiano wakati wa maonesho ya mifuko ya uwezeshaji. Matokeo ya tathmini yanaonesha **37%** ya wajasiriamali **112** walifanikiwa kufanya marejesho ya mikopo katika kipindi cha kuanzia miezi 6 hadi mwaka 1 ambapo pia mikopo ya muda huu imeonekana kuwa chaguo sahihi kwa wajasiriamali wadogo sana na wadogo kutokana na kujishughulisha na aina za biashara zisizo na mitaji mikubwa.

**Mchoro Na. 11: Muda wa Marejesho ya Mikopo**





Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji, NEEC (2023)**

Aidha, **20%** ilionesha kuwa mikopo ilirejeshwa ndani ya kipindi cha kuanzia miezi 3 hadi 6 licha ya baadhi ya mikopo hiyo kutozwa riba kubwa na aina ya mikopo hii imenufaisha zaidi wanavikundi. Muda wa marejesho wa kuanzia mwaka 1 hadi miaka 3 uliainishwa na wajasiriamali 21 sawa na **19%** ya wajasiriamali huku **16%** ikikiri kufanya marejesho ndani ya miezi 3 wakati **8%** ikionekana kunufaika mikopo ya muda mrefu ya kuanzia kipindi cha muda wa miaka 3 na zaidi. Tathmini inaonyesha mikopo ya muda mrefu inatolewa kwa wajasiriamali wa wenye mitaji ya kuanzia Tshs **5,000,000** hadi **200,000,000** na kuanzia **200,000,000** hadi **800,000,000.**

### 3.2.1.8 Ajira za Biashara za Wajasiriamali

Matokeo ya tathmini kwa sampuli ya wajasiriamali **112** waliohojiwa wakati wa maonesho yanaonesha jumla ya ajira za moja kwa moja **627** (wanawake **439** na wanaume **188**) zilizalishwa na wajasiriamali. Ajira hizi zimeainishwa kwa kuzingatia mgawanyo wa ajira wa Sera ya Biashara Ndogo Ndogo ya mwaka 2003 ambapo ajira **396** (wanawake **277** na wanaume **119**) zilizalishwa katika kundi la biashara ndogo sana waajiriwa 1 – 4 na kufuatiwa na kundi la ajira 5 – 49 ambapo jumla ya ajira **184** (wanawake **132** na wanaume **52**) zilizalishwa. Kundi la ajira za biashara za kati 50 – 99 lilifanikiwa kuzalisha ajira **47** (wanawake **33** na wanaume **14**) licha ya kuwa na ushiriki hafifu ya wajasiriamali kama mchoro unavyoonesha hapa chini.

**Mchoro Na. 12: Hali ya Ajira katika Biashara za Wajasiriamali**




Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji, NEEC (2023)**

### 3.2.2 WATOA HUDUMA ZA UENDELEZAJI WA BIASHARA NA FEDHA

Maonesho yalihudhuriwa na taasisi za utoaji wa huduma za biashara (BDS Providers) ambazo zinatoka sekta ya Umma **sita (7)** na Binafsi **(1).** NEEC iliratibu mafunzo kwa wajasiriamali kwa kushirikiana na BDS Providers ili kujenga uwezo kwa wajasiriamali kufahamu fursa na huduma mbalimbali ambazo zinalenga urasimishaji na kuongeza wigo mpana wa wananchi kulipa kodi kama msingi wa maendeleo kwa nchi. Aidha, tathmini imeainisha matokeo ya tathmini iliyofanyika kwa watoa huduma za biashara **nane (8)** ambao wanatoka katika taasisi mbalimbali wezeshi.


#### (a) Aina ya Huduma za Taasisi Wezeshi





Tathmini iliainisha aina za huduma ambazo zilipatikana na kutolewa na taasisi zilizoshiriki. Huduma hizo zilizoainishwa ni pamoja na mafunzo, ushauri elekezi utafiti, udhibiti, ufunguzi wa akaunti na taratibu za upatikanaji wa mikopo, ruzuku, dhamana, na nyinginezo. Washiriki hususan wajasiriamali walijengewa uwezo na taasisi mbalimbali za utoaji huduma za biashara. Jumla ya taasisi 8 ambazo ni *OSHA, BRELA, SIDO, TRA, Azania Bank, TBS, NSSF na GS 1 TZ* zilitoa mafunzo kwa wajasiriamali na kuwezesha kunufaisha kwa njia ya mafunzo jumla ya wajasiriamali **182** sawa na **98.4%** ya wajasiriamali walisoshiriki maonesho. Aidha, tathmini inaonesha kuwa wanawake walioshiriki mafunzo ni **108** na wanaume ni **71**na walemavu **3**. Matokeo ya tathmini yanaonesha jumla ya taasisi za fedha **13** zilionekana kujihusisha na utoaji wa mikopo,

taasisi **4** zinatoa dhamana ya mikopo na za ruzuku zilikuwa ni **2**. Tathmini ilibaini taasisi za mafunzo zilikuwa **12** sanjari na taasisi za **7** za utafiti na ushauri elekezi huku taasisi za udhibiti zikiwa ni **2** na taasisi nyingine mbili za kuzuia na kupambana na rushwa (TAKUKURU) na kundi la waratibu wa madawati ya kama jedwali na mchoro unavyooesha hapa chini.

**Michoro Na. 13: Aina ya Huduma za Taasisi katika Maonesho**





Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji, NEEC (2023)**

**(b) Maombi ya Mikopo na Dhamana**

Matokeo ya tathmini yanaonesha kulikuwa na jumla ya maombi ya mikopo **77** kwa kutoka kwa wananchi waliotembelea mabanda ya maonesho hususani taasisi za fedha. Jumla ya maombi ya mikopo yenye thamani ya Tshs **462,364,000** yalipokelewa na benki za CRDB Bank na Azania Bank. Maombi ya mikopo ambayo yanahitaji kufanyiwa tathmini ya mikopo kwa taasisi za fedha yamechambuliwa kwa uwiano wa mgawanyo wa asilimia kama ifuatavyo; CRDB **(11%),** TADB **(13%),** Azania **Benki (16%),** PASS TRUST **(14%),** SELF MF **(11%),** NEDF (9%), SCG **(3%)** na TaFF **(3%).** Mbali na maombi hayo, jumla ya wananchi **203** walifanikiwa kufungua akaunti katika mabenki huku wananchi **127** wakifungua akaunti CRDB Bank na wananchi **76** wakifungua akaunti Azania Bank kama michoro hapa chini inavyoonesha mnyumbulisho huo.

Aidha, tathmini inaonesha mwamko kwa wanawake umeongezeka katika ushiriki huku ikishuhudiwa zaidi ya **59%** ya waliofungua akaunti za benki wakiwa ni wanawake. Huduma nyingine Maonesho ya uwezeshaji yamekuwa na tija kubwa kuwafikia wananchi na kuwaunganisha na fursa za watoaji wa huduma za biashara, urasimishaji na kuwezesha wananchi kufahamu taratibu za maombi ya mikopo na urejeshaji wa mikopo kwa wakati. Hivyo, wadau na taasisi wezeshi ni vyema kuhamasishwa ili kuongeza ushiriki wa taasisi zenye tija na malengo ya kuwafikia wananchi wenye uhitaji wa kuwezeshwa kiuchumi.

**Mchoro Na. 14: Maombi ya Mikopo na Dhamana**




Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji, NEEC (2023)**

Aidha, tathmini inaonesha jumla ya mifuko ya uwezeshaji **10** na programu **moja** kati ya mifuko na programu za uwezeshaji **73** sawa na **15%** ilishiriki maonesho**.** Hivyo, kuna umuhimu mkubwa ya kuhamasishwa mifuko na programu za uwezeshaji ili ziweze kushiriki kwa wingi na kutoa elimu na fursa za uwezeshaji kwa wananchi ili kunufaika na fursa mbalimbali kama vile ruzuku, dhamana na mikopo.

# SURA YA NNE

## 4. MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA UTATUZI WA CHANGAMOTO

Mafanikio na changamoto za jumla za maonesho zimeainishwa kwa kuzingatia kundi la wajasriamali, watoa huduma za biashara, mifuko ya uwezeshaji na waratibu wa madawati ya uwezeshaji ngazi za mikoa na halmashauri kama ifuatavyo:

### 4.1 MAFANIKIO YA MAONESHO

Maonesho pamoja na mambo mengine yamekuwa na mafanikio mengi licha ya uwepo wa changamoto ambazo zimekuwa zikifanyiwa kazi ili kuongeza ufanisi wa maonesho. Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na haya ambayo yameainishwa katika jedwali hapa chini:

| Wajasiriamali | Mifuko na Programu za Uwezeshaji |
|---|---|
| (a) Kuongeza idadi ya wateja na wigo wa masoko<br>(b) Wajasiriamali **182** walinufaika na mafunzo ya urasimishaji wa biashara ili ziweze kutambulika na mamlaka husika za usajili<br>(c) Kunufaika na mafunzo ya urasimishaji wa biashara<br>(d) Kufahamu fursa za mifuko na programu za uwezeshaji<br>(e) Kufungua akaunti katika mabenki. Jumla ya akaunti za biashara 203 za wajasiriamali **33** na wananchi **170** zilifunguliwa | a) Ushiriki wa mifuko ya uwezeshaji inayotoa mikopo moja kwa moja **(13),** dhamana **(4),** ruzuku **(2)** na programu (1). Maonesho yalihusisha mabenki **3**<br>b) Jumla ya mikopo yenye thamani ya shilling **315,000,000** ambapo SELF MF ilitoa shilingi **140,000,000** na SANVN Viwanda Scheme ilitoa **175,000,000**<br>c) Mifuko kutoa mafunzo kwa wajasiraiamali na kujenga uelewa wa fursa za bidhaa za mifuko ya uwezeshaji kwa wananchi katika jitihada za kukuza wigo wa masoko |

| Watoa Huduma za Biashara | Waratibu wa Madawati ya Uwezeshaji |
|---|---|
| (a) Elimu na mafunzo ya uhamasishaji wa urasimishaji wa biashara kwa wajasiriamali na wananchi kwa ujumla<br>(b) Wananchi na wafanyabiashara kujisajili na mamlaka za usajili na urasimishaji<br>(c) Uwepo wa watoa huduma za biashara na urasimishaji ambao ni BRELA, GS 1 TZ, TRA, TBS, | (a) Jumla ya waratibu **30** walishiriki maonesho.<br>(b) Kushirikisha wadau wengi zaidi (makampuni ya simu) na maandalizi yawe mapema, uhamasishaji wa jamii (sensatization) uongezeke ili ushiriki uwe kwa kiwango kikubwa, kuongezwa vikundi vya burudani/mziki,<br>(c) Kuboresha mazingira ya uwanja wa maonesho |

| | | |
|---|---|---|
| | NSSF, SIDO, FCC n.k. | (landscaping/kufyeka majani ili kuepuka jua na joto), |
| | | |

Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji, NEEC (2023)**

### 4.2 CHANGAMOTO ZA JUMLA NA UTATUZI WA HIZO CHANGAMOTO

Tathmini imebainisha pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi, bado kuna changamoto za jumla zinazokabili uwezeshaji wananchi na kusababisha mzunguko wa umaskini katika jamii. Changamoto hizo pamoja na mambo mengine zinazokabili mifuko na programu za uwezeshaji ni:

- Kiwango kidogo cha upatikanaji wa huduma za fedha katika maeneo ya pembezoni na vijijini. Hali hii inakwamisha wafanyabiashara waliowekeza maeneo ya pembezoni na vijijini kushindwa kupanua biashara na wananchi kushindwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi.

- Elimu ya uwekezaji katika masoko ya mitaji bado ni changamoto kwa wananchi katika ununuzi wa hisa na uwekezaji wa hatifungani.

- Ukosefu wa mitaji kwa wananchi wanaohitaji kuanzisha au kukuza biashara kutokana na ukosefu wa dhamana.

- Gharama kubwa ya upatikanaji wa huduma za fedha kutokana na riba kubwa na kufanya gharama kubwa za upatikanaji wa mikopo.

- Kutorejeshwa kwa mikopo hasa inayotolewa na Mfuko wa Kuwawezesha Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kupitia asilimia 10 za mapato ya ndani ya Halmashauri.

- Ukosefu wa maeneo ya kufanyia biashara yenye mazingira wezeshi kwa ajili ya wafanyabiashara hasa wafanyabiashara wadogo.

- Ukosefu wa dhamana kwa wananchi wakiwemo wajasiriamali wadogo na wa kati kutokana na eneo kubwa la ardhi nchini kutopimwa au kurasimishwa. Ardhi ni chombo cha uwezeshaji kwa kutumika kama dhamana ya mikopo.

Changamoto nyingine zilizoainishwa zimeainishwa katika bango kitita hapa chini kwa kuzingatia kundi la wajasiriamali, mifuko na programu za uwezeshaji, watoa huduma za biashara na waratibu wa madawati ya uwezeshaji:

| S/Na. | Kundi | Changamoto | Utatuzi wa Changamoto |
|---|---|---|---|
| 1. | **Wajasiriamali** | • Idadi ndogo ya wajasiriamali walioshiriki ambapo maonesho ya Kigoma washiriki waoneshaji walikuwa **185** kwa mwaka 2023 ikilinganishwa na maonesho ya | Elimu na mafunzo endelevu ya ujasiriamali na ubunifu yaendelee kuratibiwa na kutolewa kwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | mkoani Morogoro ambapo wajasiriamali walikuwa **243** mwaka 2022.<br><br>• Mwamko mdogo wa wajasiamali katika urasimishaji wa biashara za wajasiriamali katika taasisi za urasimishaji ikiwa ni pamoja na usajili wa biashara, nembo ya msimbo milia, alama za ubora, namba ya mlipa kodi.<br><br>• Bado uelewa ni mdogo wa wajasiriamali kuhusu ujasiriamali na ubunifu wa kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa.<br><br>• Kutokuwepo kwa mkakati wa mkoa katika kuratibu matangazo ambayo yanapaswa kufanyika mwezi mmoja kabla ya maoensho.<br><br>• Uwepo wa taasisi chache wezeshi za uwezeshaji zilizo shiriki<br><br>• Uchache wa wateja wa kununua bidhaa katika mabanda ya wajasiriamali<br><br>• Gharama za kulipia mabanda hazikuwa rafiki kwa wajasiriamali hususani biashara ndogo sana | wajasiriamali na wataalam wa utoaji wa huduma za biashara kwa kuzingatia mahitaji ya mafunzo.<br><br>Matangazo ya uhamasishaji ngazi ya mkoa yashirikishe viongozi wa dini ili kuwezesha taarifa kuwafikia waumini wa dini.<br><br>Baraza lihakikishe maonesho ya mwaka 2024 yanahusisha wajasiriamali wengi pamoja ongezeko la taasisi wezeshi mabenki, mifuko na programu za uwezeshaji, NGOs na CSOs<br><br>Gharama za mabanda pia ziangaliwe kwa wajasiriamali wadogo ili waweze kushiriki kwa wingi |
| **2.** | **Mifuko na Programu za Uwezeshaji** | • Ushiriki hafifu wa wadau wa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi katika maonesho ya mkoa wa Kigoma ambapo ushiriki unaonesha wadau wa mifuko walikuwa ni 15% ya mifuko yote 73.<br><br>• Idadi ndogo ya mahudhurio ya wananchi kwa siku ikilinganishwa na idadi ya wananchi waishio mkoani Kigoma | Kujenga uelewa juu ya huduma zitolewazo na Mifuko na programu za uwezeshaji pamoja na kuongeza mtandao wa Ushirikiano baina ya taasisi telekezi. |
| **3.** | **Watoa Huduma za Biashara** | • Mwitikio mdogo wa ushiriki wa Asasi za Kiraia (CSOs) na Mashirika Yaisyo ya Kiserikali (NGOs). Wadau wengine ambao ushiriki wao ulikuwa hafifu ni Miamvuli ya Vikundi vya Kijamii vya Kifedha. | Mawasiliano yafanyike ili maonesho yajayo yaweze kuwa na ushiriki wa NGOs, CSOs, Miamvuli ya vikundi vya Kijamii vya Kifedha. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | • Mazingira ya darasa la mafunzo kwa wajasiriamali hayakuwa rafiki na hivyo watoaji wa huduma kushindwa kutumia vifaa kama vile projekta wakati wa mafunzo.<br>• Matangazo ya maonesho kutokufikia maeneo mengi ya pembezoni mwa mkoa.<br>• Kutoonekana kirahisi *Layout* ya mabanda yaliyokuwa nyuma ya mabanda ya mbele. | *Layout* ya mabanda inapaswa kuboreshwa zaidi maonesho yajayo |
| **4.** | **Waratibu wa Madawati ya Uwezeshaji** | • Barua za mialiko kutoka NEEC za maonesho kuchelewa kufika kwa wakati kunachangia ushiriki hafifu wa waratibu wa madawati ya uwezeshaji.<br>• Kutokuwepo kwa matangazo ya kutosha kunachangia kutowafikia wananchi waishio vijijini.<br>• Kutokuwepo kwa dhamana kwa vikundi ambavyo vinanufaika na 10% ni sababu inayochangia ucheleshaji wa marejesho ya mkopo.<br>• Waratibu wa madawati ya uwezeshaji kutokupewa shughuli za kufanya wakati wa maonesho<br>• Vituo vya Uwezeshaji 20 vimeanzishwa katika mikoa 8 kati ya mikoa 26 ya Tanzania Bara. | • Maonesho yafanyike kati ya Julai - Septemba kila mwaka baada ya kumalizika kwa msimu wa mavuno ya mazao ya kilimo<br>• Waratibu wa madawati ya uwezeshaji wapewe majukumu ya kufanya na NEEC wakati wa maonesho<br>• Serikali kuangalia namna ya kufanya maboresho ya usimamizi wa 10% ya mapato ya halmashauri ili kuongeza tija na ufanisi<br>• Ufuatiliaji wa mikoa ufanyike kupitia OR-TAMISEMI ili kuwezesha uanzishwaji wa vituo vya uwezeshaji kwenye mikoa 26 |

Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji, NEEC (2023)**

# SURA YA TANO

## 5. HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 HITIMISHO

Maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji mkoani yamekuwa na mafanikio makubwa licha ya kukabiliana na baadhi ya changamoto zilizoainishwa katika ripoti hii. Maonesho yamejidhihirisha kuwa ni muhimu katika kuelimisha umma kuhusu jitihada zinazofanyika katika uwezeshaji wananchi kiuchumi. Tathmini pamoja na mambo mengine imeainisha mambo ya msingi ya kujifunza katika maonesho mifuko na programu za uwezeshaji kama ifuatavyo:

(a) Jumla ya wajasiriamali **182** wanawake wakiwa ni **108,** wanaume **71** na walemavu **3** walinufaika na fursa za mafunzo yaliyoratibiwa na NEEC na kushirikisha wataalam wa utoaji wa huduma za biashara (BDS Providers) na fedha kwa lengo la kujenga uelewa mpana wa wajasiriamali. Manufaa ya mafunzo hayo pamoja na mambo mengine ni kuhamasisha urasimashaji wa biashara, huduma za usajili na upatikanaji wa mikopo, dhamana na ruzuku. Maonesho yalishuhudia wajasiriamali ambao walifungua akaunti mpya katika mabenki. Hivyo, maonesho yamekuwa na manufaa na matokeo chanya kwa wananchi pia kufanikiwa kufungua akaunti, kusajili biashara, kufahamu masharti, vigezo na taratibu za mikopo, dhamana na ruzuku.

(b) Mikopo yenye thamani ya Tshs **315,000,000** ilitolewa kwa wajasiriamali wawili kutoka katika taasisi ya fedha ya SELF Microfinance Limited ambayo ilitoa Tshs **140,000,000** kwa taasisi ya kifedha iliyopo mkoani Kigoma na SANVN Viwanda Scheme iliyotoa Tshs **175,000,000** kwa mjasiriamali mmoja kutoka Dar es Salaam.

(c) Ushirikishwaji wa viongozi wa serikali, siasa, wanamuziki maarufu na kijamii pamoja na vyombo vya habari ni muhimu kufanyika ili kuwafikia wananchi.

(d) Kuna haja ya NEEC ya kuweka bajeti ya ununuzi wa mahema (tents) ili kupunguza gharama za ukodishaji kila mwaka wakati wa maonesho ya mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi.

(e) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya wanufaika wa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi pamoja na kufanya tathmini kubaini mafanikio, changamoto na fursa za mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa mwaka 2017 – 2023

(f) Maonesho yajayo ya mifuko na programu za uwezeshaji yamepangwa kufanyika mwezi Septemba, 2024 mkoani Singida

Hivyo, maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji mkoani Kigoma yamechangia kuwaunganisha wajasiriamali na fursa za mafunzo, mikopo, teknolojia, taarifa. Sanjari na hayo, maonesho kwa namna moja ama nyingine yamewezesha wajasiriamali

kujifunza mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na masuala ya ubunifu wa bidhaa pamoja na kukuza mitandao ya wajasiriamali.

## 5.2 MAPENDEKEZO

Mapendekezo na maoni yaliyotolewa na washiriki wa maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji wakati wa zoezi la tathmini yameainishwa kulingana na makundi matatu ambayo ni wajasiriamali, watoa huduma za biashara, mifuko na programu za uwezeshaji kama ifuatavyo:

### 5.2.1 WAJASIRIAMALI

(a) Matangazo ya maonesho yatolewe mapema kwa wajasiriamali wa mijini na vijijini na ushirikishwaji wa wasanii iongezwe
(b) Maonesho yashirikishe kwa wingi wajasirimali wadogo, wa kati na wakubwa ili kujenga muunganiko wa mitandao ya kibiashara
(c) Gharama za mabanda ziko juu kwa wajasiriamali wenye mitaji midogo hivyo wanaoiomba NEEC kupunguza ili kuwezesha ushiriki wa wajasiriamali kwa wingi.
(d) Maonesho yafanyike ngazi za wilaya pia na muda wa kufunga mabanda uongezwe
(e) Matangazo ya uhamasishaji yatolewe mapema kwa Wananchi na wajasiriamali kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kabla ya maonesho.
(f) Halmashauri ziwagharimie usafiri Wajasiriamali ili waweze kujifunza na kushiriki kwa wingi.

### 5.2.2 MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI

(a) Maonesho yafanyike kila mkoa ili wananchi walio wengi wanufaike na fursa za uwezeshaji.
(b) Uhamasishaji wa maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji ufanyike kupitia jukwaa la wasanii.
(c) Muda wa kufunga maonesho uongezwe na matangazo yafanyike pia katika makanisa na misikiti. Matangazo yatolewe ya kutosha kabla ya maonesho na viongozi wa dini washirikishwe hususani wale ambao ni wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama ili kuhamasisha ushiriki wa wananchi walio wengi kupitia ibada zinazofanyika.
(d) Taarifa za maonesho zitolewe mapema na wananchi waelimishwe umuhimu wa maonesho. Wananchi wajengewe hamasa ili wanufaike na watoa huduma walioshiriki.
(e) Maonesho yashirikishe wadau walio wengi ili kuyafanya yawe na sura ya kitaifa au kikanda katika kuwafikia wananchi.

### 5.2.3 WARATIBU WA MADAWATI YA UWEZESHAJI

(a) Maonesho yafanyike baada ya kumalizika kwa msimu wa mavuno ya kilimo ili kuwapa fursa wakulima na wanunuzi kushiriki ipasavyo maonesho. Waratibu walishauri maonesho yafanyike mara baada ya mavuno ya kilimo hususani katika kipindi cha kuanzia miezi ya Juni hadi Septemba ya kila mwaka. Hii itawezesha wajasiriamali na wananchi wengi kushiriki

(b) Halmashauri ziwagharimie usafiri Wajasiriamali ili waweze kujifunza na kushiriki

kwa wingi.

(c) Baraza linapaswa kushirikiana na wizara mama kuhakikisha ongezeko la ushiriki wa viongozi wa kitaifa, mikoa na wilaya ili kuwezesha maonesho kuongeza hamasa ya maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji. Adha, wabunge na madiwani wahamasishwe ili washiriki kwa wingi.

(d) Kanuni ya utoaji na urejeshaji wa mikopo ya **10%** iboreshwe ikiwa ni pamoja na vikundi kuweka dhamana ya mali zisizohamishika kabla ya kuchukua mikopo, kuwachukulia wanakikundi hatua za kisheria(Kuwapeleka Mahakamani) endapo watashindwa kurejesha mkopo kwa wakati, Elimu ya mikopo iendelee kutolewa kwa wanavikundi na wanasiasa ili wasichanganye mikopo na siasa, Ofisi ya utoaji na urejeshwaji wa mikopo ya **10%** iwe inajitegemea katika ngazi ya Halmashauri pamoja na Umri wa vijana uongezwe kutoka miaka 35-45.

(e) Wasanii maarufu na wenye mvuto kwa jamii washirikishwe ili kuleta hamasa za wananchi kushiriki kwa wingi katika maonesho yajayo. Aidha, pia ni muhimu kuwashirikisha viongozi wa dini na madhehebu ili matangazo yawafikie waumini na wananchi kwa ujumla wake.

(f) Mapendekezo mengine yaliyotolewa na waratibu wa madawati ya uwezeshaji wananchi kiuchumi yameainishwa katika jedwali hapa chini

**Mapendekezo Mengine**

| Na. | Mapendekezo Mengine | |
|---|---|---|
| | ***Upatikanaji wa Taarifa za maandalizi ya ushiriki wa maonesho*** | • Barua za mialiko zitumwe mapema na ufuatiliaji ufanyike wa mara kwa mara kwa washiriki ili ushiriki wa taasisi wezeshi uongezeke.<br><br>• Barua za mwaliko kwa Waratibu wa Uwezeshaji Wananchi kiuchumi zitolewe mapema kwa Wakurugenzi. |
| | | Matangazo ya uhamasishaji yatolewe mapema kwa Wananchi na wajasiriamali kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kabla ya maonesho. Taarifa pia zitumwe kwa njia za vyombo vya habari na nyinginezo zitumwe moja kwa moja kwa taasisi husika, na maandalizi yapishane na maonesho mengine yanayofanyika kwa wakati mmoja mfano, (NACTVET) ili kuongeza ushiriki wa wadau wa elimu ya vyuo vikuu. |
| | | Uhamasishaji na matangazo ufanyike kwa kushirikisha viongozi wa serikali, siasa na kijamii, vyombo vya habari vitumike katika kuufahamisha Umma juu ya Maonesho, kutumia wanamuziki maarufu kuvutia wananchi *Mf. Diamond Platinums, Alikiba*. |
| | ***Gharama za Wajasiriamali katika Mcha Maonesho*** | • Gharama kubwa za mabanda.<br>• Matangazo ya uhamasishaji yafanyike pia katika nyumba za Ibada makanisani na misikitini. |

| | | |
|---|---|---|
| | ***Ulinzi na Usalama*** | Viongozi wa kitaifa, mikoa na halmashauri, wabunge, madiwani pamoja na wadau wa sekta binafsi waombwe kuhudhuria kwa wingi ili kuhamasisha ushiriki wa wananchi. |
| | | Maonesho yanapaswa kuzingatia muda wa kufunga na kufungua na ia kuwe na regista za makabidhiano jioni na asubuhi |
| | | Kuishirikisha kikamilifu kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa katika kulinda maonesho, bidhaa na usalama wa wananchi. Aidha, washiriki walishauri ulinzi uzidi kuimarishwa na walinzi wawepo muda wote wa maonesho. |
| | | Maliwatoli (vyoo) vinavyotumika katika maonesho viwe vya kudumu ili kuepusha usumbufu na magonjwa ya mlipuko. |
| | **Uendelevu wa Maonesho wa Mifuko na Programu za Uwezeshaji** | Maonesho yafanyike kila mkoa ili kutoa fursa ya ushiriki mzuri wa wananchi. |
| | | Maonesho yaendelee kutolewa kila mwaka na muda wa maonesho uongezwe na kuwa wiki mbili badala ya wiki moja. |
| | | Uratibu wa maonesho uboreshwe kwa kuweka vitu vya vinavyovutia mfano, maonesho yawe ya kitaifa badala ya kuwa ya kikanda kwa kuzingatia kuwa maonesho hayo yanafanyika mara moja kwa mwaka. |
| | | Maonesho yaendee kuwepo kuleta elimu ya mifuko na program,Mifuko ibuni vyanzo vipya vya Mapato,Mifuko inayotegemea ruzuku iwezeshwe,Kuwepo success stories ili kuleta hamasa na elimu juu ya mifuko,changamoto zinazowasilishwa zifanyiwe kazi ili kuimarisha mifuko na progam za Uwezeshaji na Mafunzo kwa Waratibu wa Madawati ya uwezeshaji wananchi kiuchumi(DECO) katika ngazi za mikoa na halmashauri. |

Chanzo: **Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji, NEEC (2023)**

## 6. VIAMBATISHO

***Kiambatisho Na. 1:***

### KIAMBATISHO Na. 1: FOMU YA TATHMINI –MJASIRIAMALI/MSHIRIKI WA MAFUNZO

1. JINSIA a. KE b. ME

2. KIWANGO CHA ELIMU
   (a) Sijasoma (b) Darasa la 7 (c) Kidato cha 4 (d) Kidato cha 6 (e) Vyuo (f) Chuo Kikuu

3. MAFUNZO *(sehemu ya mafunzo ijazwe tu na walioshiriki mafunzo wakati wa maonesho)*

Je, umewahi kushiriki na kuhudhuria mafunzo yeyote ya ujasiriamali hapo awali (a) Ndiyo (b) Hapana

Taja taasisi iliyotoa hayo mafunzo________________________________________________

Mada hayo yalihusu mada zipi? ________________________________________________

Mrejesho wa Mafunzo Yalitolewa katika Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji

| S/Na. | Eneo | Ndiyo (tiki) | Hapana (tiki) | Kiwango cha Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mafunzo yamekidhi matarajio yangu | | | |
| 2 | Nitaweza kutumia maarifa ya mafunzo niliyojifunza | | | |
| 3 | Malengo ya mafunzo kwa kila mada yaliainishwa na kufuatwa na mwezeshaji | | | |
| 4 | Maudhui ya mafunzo yalipangwa na ilikuwa rahisi kuyafuatilia | | | |
| 5 | Nyenzo (materials) zilizotolewa zilikuwa muhimu | | | |
| 6 | Wawezeshaji wa mafunzo walikuwa na maarifa na wenye ujuzi | | | |
| 7 | Muda ulitolewa wa kutosha wa maswali na majadiliano - Ushirikishwaji | | | |
| 8 | Muda wa mafunzo ulikuwa kutosheleza | | | |
| 9 | Ukumbi wa mafunzo ulikuwa mzuri kwa aina ya mafunzo yaliyotolewa | | | |
| 10 | Ni vipengele vipi vya mafunzo vinaweza kuboreshwa? | | | |

4. AINA YA BIASHARA UNAYOJISHUGHULISHA
   (a) Mazao ya Usindikaji (b) Biashara Ndogo ndogo (c) Ufumaji na ushonaji
   (b) Tafadhali ainisha nyinginezo____________________________________________

   Biashara ipo katika sekta ipi____________________________________________

5. BIASHARA ULIANZA LINI?
   (a) Ndani ya mwaka mmoja (b) zaidi ya mwaka 1 – 3 (c) zaidi ya miaka 3 – 5
   (c) Zaidi ya miaka 5

6. USAJILI NA URASIMISHAJI WA BIASHARA

6.1 Je, huwa unatoa risiti pale unapouza bidhaa za biashara yako (a) Ndiyo (b) Hapana
Kama hapana taja hizo sababu________________________________________________

6.2 BIASHARA YAKO IMESAJILIWA (a) Ndiyo (b) Hapana
6.2.1 Kama ndiyo imesajiliwa na taasisi zipi kati ya hizi zifuatazo:
(a) BRELA (b) Halmashauri (c) Tafadhali ainisha nyinginezo (kama ipo) ____________________
Je, biashara yako inatambulika na viwango vya TBS (a) Ndiyo (b) Hapana
Je, biashara yako imepata msimbomilia (Bar Code) (a) Ndiyo (b) Hapana

Je, biashara yako ina usajili wa namba ya mlipa kodi (TIN) (a) ndiyo (b) Hapana
Kama hapana, je unafahamu taratibu za kupata TIN na Msimbomilia (a) ndiyo (b) Hapana
Nini maoni kuhusu uboreshaji wa utoaji wa Namba ya Mlipa Kodi, Msimbo milia____________________

6.2.2 Kama ni hapana toa sababu za biashara kuwa katika mfumo usio rasmi____________________

7. MTAJI WA BIASHARA

| Aina ya shughuli | Mtaji wa biashara/ shughuli /kampuni | Mtaji wa Kisera |
|---|---|---|
| Biashara ndogo sana | | Hadi milioni 5 |
| Biashara ndogo | | Zaidi ya milioni 5 hadi Milioni 200 |
| Biashara ya kati | | Zaidi milioni 200 hadi milioni 800 |
| Biashara kubwa | | Zaidi ya milioni 800 |

7.1 CHANZO CHA MTAJI:
(a) Binafsi (b) Ndugu na marafiki (c) Mkopo (d) Kikundi (e) Ainisha chanzo kingine ____________
Kama ni mkopo ulitolewa na taasisi ipi?____________________
Je umewahi kukopa tena (a) Ndiyo (b) Hapana kama ni ndiyo taja hiyo taasisi____________________

7.2 MUDA WA MAREJESHO WA MKOPO
(a) ndani ya miezi 3 (b) Miezi 3 – 6 (c) Miezi 6 hadi mwaka 1 (d) mwaka 1 – 3 (e) Miaka 3 na zaidi

8. TAARIFA ZA MAONESHO YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI ULIZIPATA KUPITIA CHANZO KIPI
(a) Vyombo vya habari (b) Redio (c) TVs (d) Mitandao ya Kijamii (e) Tafadhali ainisha vyanzo vingine____________

9. MTAJI WA BIASHARA ULIKUWAJE
Wakati unaanza ___________(mwaka______) na Mtaji wa sasa umefikia kiasi gani ____________________

10. AJIRA

| Aina ya Biashara/shughuli | Ajira za biashara/ shughuli /kampuni | Ajira za Kisera | Ajira za Biashara za Wajasiriamali |
|---|---|---|---|
| Biashara ndogo sana | | 1 – 4 | |
| Biashara ndogo | | 5 – 49 | |
| Biashara ya kati | | 50 – 99 | |
| Biashara kubwa | | 100+ | |

10.1 Biashara/shughuli yako imeajiri watu wangapi?______________________________________________________________________

11. Maonesho ya mifuko na program za uwezeshaji yamekusaidiaje kama mjasiriamali ________________________________________
12. Taja changamoto ambazo umekutana nazo katika maonesha haya
_______________________________________________________________

13. Maoni/mapendekezo kuhusu uboreshaji wa maonesho ya mifuko na program za uwezeshaji kwa mwaka 2023?___________________________

## KIAMBATISHO Na. 2: FOMU YA TATHMINI – MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI

1. JINA LA TAASISI/MFUKO/PROGRAMU ______________________________
2. AINA YA TAASISI
   (a) Umma (b) Binafsi (c) Asasi za Kiraia (d) NGOs (e) Tafadhali ainisha nyingine ____________________________

3. HUDUMA ZINAZOTOLEWA
   (a) Mafunzo
   (b) Ushauri Elekezi,
   (c) Utafiti
   (d) Udhibiti
   (e) Mikopo
   (f) Ruzuku
   (g) Dhamana
   (h) Nyingine (Tafadhali Ainisha)_____________________________________

4. HUDUMA ZA WANANCHI WALIOHUDUMIWA KATIKA BANDA LAKO LA MAONESHO

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 21/5/2023 | Jinsi | | | 22/5/2023 | Jinsi | | | 23/5/2023 | Jinsi | | |
| | Me | Ke | Jumla | | Me | Ke | Jumla | | Me | Ke | Jumla |
| | | | | | | | | | | | |
| 24/5/2023 | Jinsi | | | 25/5/2023 | Jinsi | | | 26/5/2023 | Jinsia | | |
| | Me | Ke | Jumla | | Me | Ke | Jumla | | Me | Ke | Jumla |
| | | | | | | | | | | | |
| 27/5/2023 | Jinsi | | | 28/5/2023 | Jinsi | | | | | | |
| | Me | Ke | Jumla | | Me | Ke | Jumla | | | | |
| | | | | | | | | | | | |

Jumla _____________ (i) Ke __________ (ii) Me __________

**MIKOPO, DHAMANA NA RUZUKU**

5. MFUKO/PROGRAMU ULIANZISHWA MWAKA GANI?______________________________________________________________________

6. JUMLA YA THAMANI YA MIKOPO ILIYOTOLEWA TANGU KUANZISHWA KWA MFUKO/PROGRAMU HADI 2022/2023______________

7. MFUKO/PROGRAMU IMENUFAISHA WAJASIRIAMALI WANGAPI__________

KE ________ ME __________ Walemavu KE ______ ME _____

8. JUMLA YA MIKOPO ILIYOTOLEWA KATIKA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 ________________________________________

Idadi ya wanufaika wa mfuko/programu ___________ KE_________ ME________

9. MUDA WA MAREJESHO YA MKOPO/DHAMANA
   (i) Miezi 12
   (ii) Miezi 24
   (iii) Miezi 36
   (iv) Miezi 48
   (v) Miezi 60
   (vi) Tafadhali ainisha nyinginezo________________________________________________________________________________________

10. KIWANGO CHA MIKOPO KINACHOTOLEWA NA MFUKO/PROGRAMU
    (i) Kiwango cha chini _______________________ (ii) Kiwango cha Juu ______________

11. KIWANGO CHA RIBA CHA MFUKO/PROGRAMU
    a. Baada ya kuanzishwa _____________________________________________
    b. Kiwango kinachotozwa kwa sasa (2023) ____________________________
       Je mabadiliko ya riba yameathiri utendaji wa mfuko/program
       (a) Ndiyo (b) hapana
       Kama ndiyo taja hizo sababu ______________________________________

12. HALI YA MAREJESHO IKOJE KWA WAKOPAJI____________________________

    - Ainisha utaratibu wa marejesho ya mikopo _____________________________

13. Tangu mmeanza kukopesha je ni kiasi gani cha mkopo kimerejeshwa hadi mei 2023?________________________________________
14. Tangu mmeanza kukopesha je ni kiasi gani cha mkopo hakijarejeshwa hadi kufikia Mei 2023?__________________________________
15. Je kuna hatua zozote zilizochukuliwa kwa wadaiwa sugu (Mikopo chechefu) kwa kipindi husika?________________________________

**MAFUNZO**

16. Mfuko tangu kuanzishwa umefanikiwa kunufaisha wajasiriamali wangapi kwa njia ya mafunzo________________________________

KE___________ ME__________ Walemavu: KE________ ME____________

17. AINA YA MAFUNZO YATOLEWAYO NA MIFUKO/PROGRAMU ZA UWEZESHAJI
    i. Nadharia
    ii. Vitendo
    iii. Utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu
    iv. Uwekaji wa Akiba
    v. Uongozi Bora
    vi. Demokrasia
    vii. Tafadhali ainisha mengineyo ______________________________________________________________

18. MAFUNZO YALITOLEWA KIPINDI GANI
    (a) Kabla ya mikopo (b) Baada ya mikopo
    Nini matokeo ya mafunzo yaliyotolewa ____________________________________________________________

19. MUDA WA HAYO MAFUNZO
    (a) Siku 1 – 5 b. Wiki 1 c. Wiki 2 d. Wiki 3 e. Mwezi na zaidi

20. TAJA AINA YA MAFUNZO YALIYOTOLEWA _______________________________________________________

21. JUMLA YA MAOMBI YA MIKOPO YALIOOMBWA TANGU TAASISI/ MFUKO WAKO UANZISHE.

| s/n | Aina ya Wajasiriamali | Kiasi Walichoomba | Idadi ya Maombi | Wanuaika (KE) | Wanufaika (ME) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Wajasiriamali wadogo sana | | | | |
| 2 | Wajasiriamali wadogo | | | | |
| 3 | Wajasiriamali wakati | | | | |
| 4 | Wajasiriamali Wadogo | | | | |

22. JUMLA YA MAOMBI YALIYOPATA MKOPO. TANGU TAASISI/ MFUKO WAKO UANZISHE HADI SASA.

| s/n | Aina ya Wajasiriamali | Kiasi Walichopata | Idadi ya Wanufaika | Wanufaika KE | Wanufaika ME |
|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Wajasiriamali wadogo sana | | | | |
| 2 | Wajasiriamali wadogo | | | | |
| 3 | Wajasiriamali wakati | | | | |
| 4 | Wajasiriamali Wadogo | | | | |

23. JUMLA YA MAOMBI YALIYOKOSA MKOPO. TANGU TAASISI/ MFUKO WAKO UANZISHE HADI SASA.

| s/n | Aina ya Wajasiriamali | Kiasi Walichopata | Idadi ya Wanufaika | Wanufaika KE | Wanufaika ME |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Wajasiriamali wadogo sana | | | | |
| 2 | Wajasiriamali wadogo | | | | |
| 3 | Wajasiriamali wakati | | | | |
| 4 | Wajasiriamali Wadogo | | | | |

24. NI DHAMANA ZIPI ZINAZOTOLEWA KWA WANUFAIKA WA MIKOPO

| s/n | Aina ya Wajasiriamali | Dhamana | Thamani ya chini ya Dhamana Ya Mkopo (Collaterall) | Thamani ya Juu ya Dhamana ya Mkopo(Collateral) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Wajasiriamali wadogo sana | | | |
| 2 | Wajasiriamali wadogo | | | |
| 3 | Wajasiriamali wakati | | | |
| 4 | Wajasiriamali Wadogo | | | |

25. JE HALI YA UTOAJI MIKOPO KATIKA TAASISI YAKO?
(a) Imepungua _______ (b)Kuongezeka_______
26. Taja sababu za kupungua au kuongezeka kwa hali ya utoaji mikopo katika Taasisi yako_______________________
27. TAJA SABABU ZINAZOPELEKEA WAJASIRIAMALI KUKOSA MIKOPO KUTOKA KATIKA TAASISI /MIFUKO YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ________________________________________________________________________________________________

28. JUMLA YA AJIRA ZILIZOZALISHWA NA MFUKO/PROGRAMU TANGU KUANZISHWA HADI SASA_____________________________

1.1 KE b. ME c. walemavu

Kati ya hizo ajira: ajira za moja kwa moja ni _______________ na zisizo za moja kwa moja ni ___________________________________

29. Ainisha mafanikio uliyoyapata/uliyoyaona katika maonesho ya hapa Mkoani Kigoma__________________________________________

30. Ainisha CHANGAMOTO ulizokumbana nazo KATIKA MAONESHO MKOANI KIGOMA_________________________________________

31. MAONI YA KUBORESHA MAONESHO YA MWAKANI YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI__________________________________________________________________________________________________________________

## KIAMBATISHO Na. 3: FOMU YA TATHMINI – WATOAJI HUDUMA ZA BIASHARA (BDS) NA TAASISI

1) **JINA LA TAASISI** ______________________________________________
2) **IDADI YA WASHIRIKI (*EXHIBITORS)*** KE ______ ME______ JUMLA__________
3) **AINA YA TAASISI**
   - (a) **Umma**
   - (b) **Binafsi**
   - (c) **Asasi ya Kiraia (CSOs)**
   - (d) **Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs)**
   - (e) **Nyingine (Tafadhali Ainisha)**___________________________________

4) **HUDUMA ZINAZOTOLEWA**
   - (a) **Mafunzo**
   - (b) **Ushauri Elekezi**
   - (c) **Utafiti**
   - (d) **Udhibiti**
   - (e) **Mikopo**
   - (f) **Ruzuku**
   - (g) **Dhamana**
   - (h) **Nyingine (Tafadhali Ainisha)**___________________________________

5) **IDADI YA WANANCHI WALIOHUDUMIWA KATIKA BANDA LAKO LA MAONESHO**

| 21/5/2023 | Jinsia | | | 22/5/2023 | Jinsia | | | 23/5/2023 | Jinsia | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Me | Ke | Jumla | | Me | Ke | Jumla | | Me | Ke | Jumla |
| | | | | | | | | | | | |
| | Jinsia | | | | Jinsia | | | 26/5/2023 | Jinsia | | |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **24/5/2023** | | | | **25/5/2023** | **Me** | **Ke** | **Jumla** | | **Me** | **Ke** | **Jumla** |
| | | | | | | | | | | | |
| **27/5/2023** | **Jinsia** | | | **28/5/2023** | **Jinsia** | | | | | | |
| | **Me** | **Ke** | **Jumla** | | **Me** | **Ke** | **Jumla** | | | | |
| | | | | | | | | | | | |

**Jumla ______________ (i) Ke ___________ (ii) Me ___________**

6) **MAFANIKIO ULIYOYAPATA AU KUYAONA KATIKA MAONESHO HAYA_____________________________________________________________**
7) **CHANGAMOTO ULIZOKUMBANA NAZO KATIKA MAONESHO HAYA_______________________________________________________________**
8) **NINI KIFANYIKE ILI KUZIONDOA CHANGAMOTO HIZO ZISIJITOKEZE KATIKA MAONESHO YAJAYO (2024)______________________________**
9) **NINI MAPENDEKEZO YAKO YA JUMLA KATIKA MAONESHO HAYA KWA KUZINGATIA MAENEO YAFUATAYO**

| **Na.** | **ENEO** | **PENDEKEZO** |
|---|---|---|
| 1. | Upatikanaji wa taarifa wa maandalizi ya ushiriki wa maonesho haya | |
| 2. | Unashauri ni kipindi gani kifanyike maonesho na kwa muda wa siku ngapi? | a) Kipindi gani (msimu)<br>b) Muda wa siku ngapi |
| 3. | Unapendekeza nini kiboreshwe kwenye ulinzi na usalama katika maonesho | |
| 4. | Unashauri nini kifanyike kuleta mwamko wa wananchi kushiriki kwa wingi katika maonesho haya | |
| 5. | Nini maoni yako kuhusu uendelevu wa mifuko na program za uwezeshaji baada ya maonesho | |

## KIAMBATISHO Na. 4: FOMU YA TATHMINI – WARATIBU WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

**1. JINSI** a. Ke b. Me c. Jumla ______________

**2. KIWANGO CHA ELIMU**

(a) Kidato cha 4 (b) Kidato cha 6 (c) Vyuo vya Kati (d) Chuo Kikuu

**3. HALI YA USHIRIKI WA WARATIBU UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI KATKA MAONESHO YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI TANGU MWAKA 2018 HADI SASA.**

(a) Hafifu (b) Nzuri (c) Nzuri sana

**Asilimia ya Ushiriki wa Waratibu Uwezeshaji wananchi kiuchumi katika maonesho ya Mifuko na Program za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

| MWAKA | IDADI YA WASHIRIKI | | | MKOA WATOKAKO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| | Me | Ke | Jumla | | |
| 2020 | | | | | |
| 2021 | | | | | |
| 2022 | | | | | |
| 2023 | | | | | |
| **JUMLA** | | | | | |

**4. NINI KIFANYIKE KUBORESHA USHIRIKI WA WARATIBU WA UWEZESHAJI WANACHI KIUCHUMI KATIKA MAONESHO YA MIFUKO NA PROGRAM ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**_______________________________________________

**5. CHANGAMOTO AMBAZO ZIMEJITOKEZA KATIKA USHIRIKI WA WARATIBU KATIKA MAONESHO YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI.**_______________________________________________

6. **NINI MAONI YAKO ILI KUWEPO NA UENDELEVU NA USHIRIKI WA PROGRAMU NA MIFUKO YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI KATIKA NGAZI ZA HALMASHAURI ZA JIJI, MANISPAA, MIJI, HALMASHAURI ZA WILAYA NA MIKOA** _______________________________________________

**KIAMBATISHO Na 5: WARATIBU WA MADAWATI YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

| Na. | REGIONAL COORDINATORS | DISTRICTS COORDINATORS |
|---|---|---|
| 1. | Kilimanjaro RS | Kahama MC |
| 2. | Kigoma RS | Kinondoni MC |
| 3. | Dar es salaam RS | Muleba DC |
| 4. | Geita RS | Bukoba MC |
| 5. | | Buchosya DC |
| 6 | | Hai DC |
| 7 | | Bukoba DC |
| 8 | | Arusha CC |
| 9 | | Arusha DC |
| 10 | | Dar es salaam CC |
| 11 | | Mwanza CC |
| 12 | | Songea MC |
| 13 | | Mlele DC |
| 14 | | Njombe TC |
| 15 | | Kibaha DC |
| 16 | | Itilima DC |
| 17 | | Nyasa DC |
| 18 | | Igunga DC |
| 19 | | Misungwi DC |
| 20 | | Ifakara TC |
| 21 | | Biharamulo DC |
| 22 | | Maswa DC |
| 23 | | Misenyi DC |
| 24 | | Bariadi DC |
| 25 | | Nsalala DC |
| 26 | | Ushetu DC |